

**Dicky** Flavour aomba mashabiki 'Tuyamalize'

UKURASA 20




**Mbappe** 'aota mbawa' Madrid

UKURASA 21


# MAISHA

DESEMBA 27, 2020 Nipashe — Baba, Mama na Mwana — *Jumapili*



Ukurasa 10

**Mtoto lazima ajifunze maneno machafu**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Pazia nalo linanogesha kama pambo la nyumba



**HARUSI**

Ukurasa 12


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Desemba 27, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580442

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz  www.facebook.com/nipashetz  www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




NGOZI INAYONG'ARA

**Kitunguu maji kinatosha kukupa furaha**

UKURASA 9



## RIPOTI MAALUM

# Kutoka faru 10,000 hadi 15 tu nchini

UKURASA 4&5



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (katikati), akizungumza na Mbunge mstaafu wa Jimbo la Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi 'Sugu' (kushoto), alipotembelea hoteli ya Desderia, kuangalia uwekezaji alioufanya na kumfikishia maagizo ya Rais John Magufuli, jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Simulizi familia kuteketea kwa moto

UKURASA 2

# JPM azuia kuvunjwa hoteli ya Sugu

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play  App Store


**MICHEZO** **SIMBA YASAKA HESHIMA FA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# JPM azuia kuvunjwa hoteli ya Sugu

**Na Waandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amezuia kuvunjwa kwa hoteli ya Desderia inayomilikiwa na aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Mjini (CHADEMA), Joseph Mbilinyi, maarufu Sugu, huku akimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, kuhakikisha anasimamia na kuhakikisha jambo hilo halifanyiki.

Kabla ya Rais Magufuli kumwagiza Chalamila, kulikuwapo na taarifa za hoteli hiyo yenye hadhi ya nyota tatu, kutakiwa kuvunjwa kwa madai kuwa ilijengwa kwenye chanzo cha maji.

Chalamila jana asubuhi alifika katika hoteli hiyo na kuonana na Sugu na kumfikishia ujumbe aliotumwa na Rais Magufuli.

"Mheshimiwa Rais Magufuli amenituma nije nikueleze kwamba hakuna mtu yeyote kuja kugusa na kusema anabomoa hoteli hii kwa sababu wewe mwekezaji kama walivyo wawekezaji wengine," alisema Chalamila.

Chalamila alisema Rais Magufuli amewaagiza kuwa hata kama kuna viwanja vingine katika eneo hilo la Uzunguni ambavyo vinahitaji uwekezaji, Sugu akihitaji apewe haraka kwa vile ndiye ambaye ameonyesha nia ya kuwekeza katika eneo hilo.

Aidha, Chalamila alisema Rais Magufuli amewaonya watendaji waliokuwa na mawazo hayo ya kuvunja hoteli hiyo kwa sababu za kisiasa au kuvuruga utaratibu wa mlolongo wa kibiashara, kuacha tabia hiyo mara moja.

Chalamila pia akatumia nafasi hiyo kutoa wito kwa watu wote wenye nia ya kuwekeza, kufika mkoani Mbeya na kufanya uwekezaji wao, akidai kuwa mkoa huo una mazingira mazuri ya uwekezaji, kuanzia hali ya usalama, soko na hata upatikanaji wa malighafi.

Kwa upande wake, Sugu alimshukuru Rais Magufuli kwa ujumbe huo, akidai kuwa utasaidia wawekezaji wengine nchini kujiamini na kufanya uwekezaji zaidi.

Sugu alisema ujenzi wa hoteli hiyo umefuata taratibu zote za kisheria ikiwa ni pamoja na kupata vibali kutoka kwenye mamlaka zote za serikali.

Alisema mbali na kufuata sheria za nchi, pia hoteli hiyo imetoa ajira kwa Watanzania sambamba na kuwa mstari wa mbele katika kulipa kodi na tozo za serikali kwa mujibu wa sheria, hivyo alisikitishwa na taarifa za kutaka kuivunja.

Sugu alimweleza mkuu huyo wa mkoa kuwa hata akipata nafasi ya kufanya uwekezaji mwingine zaidi, hafikirii kwenda sehemu nyingine na badala yake atatoa kipaumbele mkoani Mbeya kwa vile anaamini panafaa kwa uwekezaji.

Hoteli ya Desderia ina huduma za malazi, vinywaji na vyakula na vyumba 16, huku gharama ya chumba kimoja ikiwa Sh. 120,000 kwa siku.

Sugu aliita hoteli hiyo jina la Desderia ambalo ni la marehemu mama yake mzazi kwa lengo la kumuenzi.

● **Imeandikwa na Nebart Msokwa, Mbeya na Enock Charles, DAR**



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (katikati), akipata maelezo kutoka kwa Mratibu wa Taasisi ya Muslim Mission, Ayn Sharif (wa pili kushoto), wakati alipotembelea kambi ya siku mbili ya utoaji wa huduma mbalimbali za macho kwa wananchi, iliyowekwa Shule ya Sekondari ya Mpendae Wilaya ya Mjini juzi. **PICHA: IKULU**

## TMA: Mvua kubwa yaja mikoa sita

**Na Enock Charles**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa (TMA), imetoa tahadhari ya kunyesha mvua kubwa kwa siku mbili katika mikoa sita na uwezekano wa kuleta athari kwa wakazi wa mikoa hiyo.

Imesema huenda mvua hiyo ikasababisha barabara kutopitika kutokana na mafuriko na baadhi ya makazi ya watu kuzungukwa na maji, hivyo kuwataka wananchi kuchukua tahadhari.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo ya TMA iliyotolewa jana, mikoa inayotarajiwa kupata mvua hiyo ni Iringa, Njombe, Lindi, Mtwara, Ruvuma na Morogoro na kwamba mvua hiyo inatarajiwa kunyesha juu ya wastani kuanzia jana.

Mamlaka hiyo pia imetoa hadhari ya uwezekano wa kuwapo mawimbi makubwa yanayofikia ukubwa wa mita mbili.

Pia, mamlaka hiyo ilitahadharisha kuwapo kwa upepo unaokwenda kasi ya kilometa 40 kwa saa utakaosababisha kuathiri shughuli za uvuvi, usafiri baharini, upatikanaji wa samaki.

Imesema upepo huo unatarajiwa kuanza Desemba kesho maeneo ya Pwani ya Bahari ya Hindi katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Dar es Salaam, Pwani na Tanga pamoja na maeneo ya Mafia, Unguja na Pemba.

Mamlaka hiyo imeshauri watumiaji wa Bahari ya Hindi kwa shughuli mbalimbali wachukue tahadhari na hatua stahiki huku wakiendelea kufuatilia hali hiyo na watoe mrejesho kwa mamlaka hiyo kila inapobidi ili hatua mbalimbali zichukuliwe. Tayari athari za mvua hizo zimeshaanza kuonekana katika Jiji la Dar es Salaam baada ya jana mchana mvua kubwa kunyesha na kusababisha madhara kadhaa, ikiwa ni pamoja na kuanguka kwa sehemu ya ukuta wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) eneo Segerea.

# Mama, watoto wawili wafa nyumba ikiungua

**Na Waandishi Wetu,** TANGA

SIMANZI imetawala katika Mtaa wa Majengo Mapya ulioko Mzingani jijini Tanga, baada ya watu watatu wa familia moja; mama na watoto wake wawili, kupoteza maisha kwa ajali ya moto, huku mumewe akijeruhiwa.

Jana, Meya wa Jiji hilo, Abdulrahman Shiloo, alisema moto huo ambao chanzo chake kinaacha maswali, ulitokea Desemba 26 mwaka huu majira ya saa 11 alfajiri.

Kwa mujibu wa Shiloo, waliofariki dunia ni Ezra Kimbi (7) na Samweli Kimbi (6) na mama yao mzazi ambaye jina lake halijafahamika.

"Hili tukio linahuzunisha sana, lakini kwa namna wananchi na majeruhi wa ajali hii walivyohangaika kuokoa maisha ya wenzetu watatu waliofariki dunia, tumepata funzo kubwa na nimegundua tuna tatizo la upatikanaji wa huduma ya haraka kwenye gari la zimamoto.

"Sasa, kama Halmashauri ya Jiji, tutachukua hatua ya kulitatua tatizo hili kwa kuhakikisha gari la zimamoto linakuwa tayari muda wote ili kurahisisha utoaji wa huduma," alisema Shiloo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Kamishna Msaidizi Blasius Chatanda, alipotafutwa kuzungumzia tukio hilo, simu yake ilikuwa ikiita bila kupokelewa.

Mashuhuda wa tukio hilo walidai kuwa wakati moto huo unaanza kuenea, baba alionekana akipiga kelele nje ya nyumba hiyo, huku mama na watoto wakiteketea ndani hadi kupoteza maisha.

Akielezea zaidi mkasa huo, Fatuma Kingo, ambaye ni mmiliki wa nyumba hiyo iliyoungua, alisema majira ya saa 11 alfajiri, alisikia kishindo kizito na baada ya muda aliona moto ukiwaka na baba wa familia hiyo akiwa nje anapiga kelele.

"Nilisikia kishindo na baadaye kidogo nikaona moto ukiwaka, lakini kimya kingi kilitanda ndani baadaye sauti ya baba ilisikika nje.

"Sasa hapa maswali yanakuja ikiwa baba alilala ndani ama la na kama alilala ndani, kwanini alishindwa kutoka na familia yake?

"Utata mwingine ni mgogoro wa kifamilia na mlango kuwa wazi wakati wa tukio hilo linatokea, ambapo inadaiwa kuwa wanafamilia hao wamekuwa na ugomvi wa muda mrefu.

"Huwa tunawaona wakigombana kwa muda mrefu, ingawa hakuna mtu aliyewahi kuingilia ugomvi wao. Kwa hiyo, hapa kila mtu ana maswali mengi," alisema.

Akisimulia mkasa huo, majeruhi ambaye ni baba mzazi wa watoto na familia hiyo, Sigifrid Kimbi (38), alisema alisikia kishindo cha mbao za paa zikianguka, lakini hakubaini kwa haraka ni nini kilikuwa kimetokea kutokana na usingizi aliokuwa nao.

"Nilisikia kishindo cha mbao za paa ya nyumba zikianguka na baadaye mtungi wa gesi ulilipuka na nguvu ya moto ikawa kubwa zaidi.

"Nyumba hiyo imekuwa na tatizo la umeme kwa muda mrefu sasa na nimeshatoa taarifa kwa mamlaka husika mara nyingi, lakini hakuna maelezo wala ufuatiliaji wa wahusika," alidai.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa huo wa Sahare, Majengo Mapya Jumanne Upepo, alisema mpaka sasa wanasubiri Jeshi la Polisi lifanye uchunguzi wa kina kumaliza utata wa chanzo cha moto huo.

Ofisa Muuguzi wa zamu aliyekuwa wodi namba saba katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga (Bombo), Mary Mngazija, alisema kuwa jana asubuhi, alimpokea Kimbi akiwa mahututi na kuwekwa kwenye chumba cha uangalizi maalum wa madaktari (ICU).

"Ni kweli tumempokea huyo majeruhi leo (jana) na anaendelea kupata matibabu chini ya uangalizi wa madaktari.

"Pia tumepokea miili mitatu ambayo ni ya mwanamke mmoja aliyefariki (dunia) kutokana na kuungua moto pamoja na watoto wawili wadogo wa kiume.

●**Imeandikwa na Lulu George na Boniface Gideon**

**NAFASI ZA SHULE**

Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.



Mbunge wa Nachingwea mkoani Lindi, Dk. Amandus Chinguile (mwenye suti), akiongozana na baadhi ya wamachinga wa stendi mpya ya mabasi ya mkoani mjini humo juzi, kwenda kusikiliza kero zinazowakabili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watu wawili wafa jengo lililoporomoka Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WATU wawili wamefariki dunia na wanne kujeruhiwa kutokana na kuporomoka kwa jengo la kihistoria, maarufu Beit al ajab.

Jengo hilo liliporomoka juzi mchana huko Forodhan mjini Unguja.

Akitoa taarifa ya ajali hiyo kwa waandishi wa habari jana, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Utaratibu na Baraza la Wawakilishi, Dk. Khalid Salum Muhammed, aliwataja waliofariki dunia kuwa ni Pande Makame Haji (25), mkazi wa Bububu, Unguja na Burhan Ali Makuno (35), mkazi wa Mtoni Kidatu mjini Unguja.

Alisema miili ya marehemu ilipelekewa katika Hospitali ya Mnazimmoja kwa ajili ya uchunguzi na kisha kukabidhiwa kwa jamaa zao kwa ajili ya maziko.

Aliwataja waliojeruhiwa ambao wako katika Hospitali ya Mnazimmoja kwa ajili ya matibabu ni Ali Ramadhan (28), mkazi wa Kinuni, Haji Juma Machano (24), mkazi wa Chumbuni, Hamad Mattar (35) na Zamir Salum (40), wote wakazi wa Kinuni.

Alisema kuwa kati ya majeruhi hao, wawili wanaendelea vizuri na wawili wako katika uangalizi maalum wa madaktari Hospitali ya Mnazimmoja mjini Unguja.

"Katika mwendelezo wa kazi za utafutaji na uokoaji jana (juzi) usiku, walipatikana watu wawili wakiwa tayari wameshafariki dunia na tayari wameshakabidhiwa kwa jamaa zao kwa ajili ya mazishi," alisema.

Alisema serikali inaendelea kusimamia kwa karibu shughuli zote za operesheni zinazoendelea kuhusiana na tukio hilo ikiwamo utafutaji na uokoaji katika eneo la tukio, uondoshaji wa kifusi na maendeleo ya matibabu kwa waliojeruhiwa.

Alivishukuru vikosi vya ulinzi na usalama, Wakala wa Barabara, Mamlaka ya Bandari na wananchi kwa ujumla kwa juhudi zao katika kufanikisha shughuli za utafutaji na uokoaji.

Hata hivyo, alisema shughuli za uokoaji katika eneo la tukio hilo bado zinaendelea na kuwataka wananchi kuendelea kuwa na subira katika kipindi hiki na serikali itaendelea kuwapa taarifa kadri shughuli za operesheni zitakavyokuwa zikiendelea hadi kukamilika kwake.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, pamoja na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, kwa nyakati tofauti walifika katika Hospitali ya Mnazimmoja kuwafariji majeruhi wa ajali ya jengo hilo, ambao wanaendelea kupatiwa matibabu.

Akizungumza akiwa hospitalini huko, Dk. Mwinyi alivitaka vyombo vya ulinzi na usalama kufanya uchunguzi wa haraka ili kubaini chanzo cha ajali ya kuporomoka kwa sehemu ya jengo hilo la makumbusho ya Taifa.

Alivitaka vyombo hivyo kufanya uchunguzi wa kina na wa haraka ili kubaini chanzo cha tukio zima la kuporomoka sehemu ya jengo hilo na kuleta maafa kwa wananchi, ili serikali ichukue hatua madhubuti na kwa haraka.

Alisema msiba uliotokea ni wa Taifa na hivyo akawapa pole wafiwa pamoja na kuwaombea dua majeruhi wa tukio hilo ili wapone haraka na kurudi katika shughuli za ujenzi wa Taifa.

Rais pia alizitaka mamlaka mbalimbali, ikiwamo Mji Mkongwe, Shirika la Nyumba na Taasisi ya Wakfu na Mali ya Amana kufanya tathmini ya haraka ya majengo yote yaliyoko katika hali mbaya, ili yafungwe na tathmini hiyo kuielekeza serikali namna ya kuyafanyia matengenezo ili kuepusha ajali kama hiyo.

Alisema serikali itagharamia maziko ya wananchi waliopoteza maisha kutokana na ajali hiyo sambamba na kuchukua hatua nyingine, ili kuhakikisha matukio ya aina hiyo hayatokei tena.

Rais Mwinyi aliwapongeza wafanyakazi wa hospitali hiyo, wakiwamo madaktari na wauguzi kwa kazi kubwa na nzuri ya kuwahudumia wagonjwa na kuwataka kuongeza juhudi.

# Mmiliki kiwanda adai kuvamiwa na kuporwa

**Na Samson Chacha,** TARIME

MFANYABIASHARA wa nafaka na mmiliki wa kiwanda kidogo cha kubangua nafaka, Hezron Moronya, amedai kuvamiwa wakati akiingia nyumbani kwake usiku na kutekwa na kundi la watu wanane waliokuwa na silaha za moto.

Amedai wahalifu hao walifyatua risasi nne hewani kisha kumpora fedha alizokuwa nazo Sh. milioni 2.3, kitabu cha hundi na simu ya mkononi kisha kutokomea kuelekea Isebania, Kenya.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki kuhusu tukio hilo, mfanyabiashara huyo:

"Mnamo Desemba 23 saa mbili usiku, nilifunga biashara yangu ya kiwandani kule Kijiji cha Sokoni hapa Sirari, nilichukua gari langu dogo kuelekea nyumbani kwangu karibu na kiwandani.

"Nilipofika nje ya lango la kuingia, nilipiga honi, familia ilifika kunifungulia lango la kuingia ndani.

"Niliposhuka kutoka ndani ya gari, nilishtuka kuwaona watu wanane wakiwa na silaha, mmoja akiwa na bastola na mwingine bunduki kubwa.

"Na hapo waliniamuru kutoa fedha zote nilizonazo na kila kitu, familia yangu ilianza kupiga kelele za kuomba msaada.

"Watu hao walifyatua risasi nne hewani kwa lengo la kuwatia hofu waliotaka kuja kutoa msaada, risasi moja ikapiga na kutoboa gari langu kwa mbele.

"Walininyang'anya fedha taslimu Sh. milioni 2.3 nilizokuwa nazo mfukoni, saa moja aina ya Infmax yenye thamani ya Sh. 280,000, kitabu changu cha Benki ya NMB na kisha kutoweka na vitu hivyo.

"Watu waliposikia milio ya risasi na kelele za kuomba msaada walijitokeza, lakini wahalifu hao walitokomea na kuvuka mpaka kuelekea Isebania nchini Kenya.

"Polisi walifika baadaye na nilikwenda kufungua jalada Kituo cha Polisi Sirari na kupewa namba SIR/IR/2142. Ninaendelea kufuatilia ili kupata msaada wa kuwakamata waliohusika na tukio hilo la kuninyang'anya fedha na vitu vyangu vingine."

Diwani wa Sirari, Amos Sagara, alisema uongozi wa kata hiyo kupitia wenyeviti wa vijiji vya Sokoni, Kanisani, Mpakani, Forodhani na Buriba na kamati zake za ulinzi wameazimia kufanya doria usiku kucha kwa kuwashirikisha wananchi, askari wa jeshi la akiba walioko katika kata hiyo na Jeshi la Polisi.

Aliliomba Jeshi la Polisi lifanye doria kwa miguu na magari kuzunguka maeneo ya mpakani hususani maeneo ya Nyamorege, Machinjioni, Sokoni na Forodhani kwa kuwa wahalifu wengi wanaotumia silaha za moto.

Kamanda wa Polisi wa Tarime/Rorya, William Mkonda, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo la uhalifu.

Alisema Jeshi la Polisi linafuatilia mtandao huo wa majambazi, akiwaomba wananchi kujitokeza kutoa taarifa ili kuwakamata watuhumiwa hao.

RIPOTI MAALUM

# Ujangili ulivyowanyofoa faru 10,000 wakabaki 15

## ■Harakati sasa zalenga wafike 200
## ■Silaha za kivita, majangili wanaswa
## ■Leo mwaka kifo cha 'bibi' Faru Fausta

**Na Sanula Athanas**

KATIKA tafsiri ya nguzo kuu za uchumi wa Tanzania, utalii una nafasi kubwa. Takwimu za Wizara ya Maliasili na Utalii zinaonesha sekta hiyo sasa inachangia robo ya fedha za kigeni na asilimia 17.5 ya Pato la Taifa.

Kadri mtu anavyozama kuuchambua utalii huo, anakutana na makundi makuu ya wanyamapori ambao ndiyo vivutio vinavyosafirisha wageni kutoka mbali kuja kuwashuhudia.

Katika makundi hayo, kuna wanyama wakubwa watano ambao ni tembo, faru, twiga, nyati na simba.

Unapomtaja mnyama faru, hapo ndipo tatizo linapoanzia. Kwanini? Wanyama hao ambao wamekuwa kivutio kikuu cha watalii, wamekuwa katika hatari ya kutoweka kiasi cha kutikisa mwelekeo wa taifa.

Wakati kuna mtazamo wa jumla, katika mustakabali wa kipekee, leo ni siku maalum kwa wadau wote wa wanyamapori na washirika wa sekta ya utalii, kwa maana ya kumbukumbu ya mwaka mmoja kamili tangu kifo cha Faru Fausta.

Huyu ni aliyekuwa faru mzee zaidi si tu kwa Tanzania, bali kwa dunia nzima akishikilia rekodi hiyo.

Ofisa Mwandamizi wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Philbert Ngoti (pichani), anasema udhalimu umewakumba wanyamapori hao hata wakapungua kutoka 10,000 waliokuwapo nchini miaka ya 1970, ndani ya miaka 30 wakabaki 15 tu.

Pia, takwimu za Shirika la Uhifadhi Duniani (IUCN), zinabainisha kuwa katika miaka ya 1970 Tanzania ilikadiriwa kuwa na faru 10,000 huku Hifadhi ya Taifa Serengeti pekee ikiwa na wanyama hao wapatao 700.

Tayari shirika hilo limeshatangaza kuwa wanyama aina ya faru weusi ambao wako 750 katika Ukanda wa Afrika Mashariki, ni miongoni mwa viumbe vilivyo hatarini kutoweka duniani.

Vilevile, Shirika la Kimataifa la Uhifadhi wa Mazingira na Wanyamapori (WWF), linabainisha kuwa Tanzania imepoteza takribani asilimia 99 ya faru weusi katika kipindi cha miaka 40 iliyopita.

Sababu ni nini? Ngoti ambaye ni Mratibu wa Faru nchini, anawanyooshea kidole majangili kuwa ni sehemu ya mzizi wa tatizo lililobadili historia ya nchi na hata kuelekea kuwa hasi zaidi.

Anasema Tanzania ni nchi iliyotamba duniani kwa idadi kubwa ya faru, lakini kutokana na baa la ujangili, iligeuka kuwa na hifadhi ya



kubahatisha ya wanyama hao, tukio la kiharamia linazozikabili pia nchi nyingi duniani.

Kutokana na hali hiyo, Ngoti anasema serikali ilichukua hatua mbili kuu, ikiwa ni pamoja na ukali uliopitiliza katika ulinzi wa wanyamapori, ambao sasa askari wake wanaowajibika ni jeshi kamili.

Anasema serikali pia iliumiza kichwa kwa njia ya pili inayotokana na faru waliopelekwa ughaibuni Afrika Kusini wakawe mahali salama na rahisi kuzaliana, wakiwa katika hesabu ya wanandugu tisa waliorejeshwa katika hifadhi za nyumbani Novemba 10 mwaka jana.

Ofisa huyo anabainisha kuwa kuchukuliwa kwa hatua hiyo ya nchi kupeana faru, ni sehemu ya utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Kusimamia Viumbe Vilivyo Hatarini Kutoweka (CITES).

Ngoti anasema kuwa katika maisha hayo mapya, faru hao waliotoka ughaibuni na ndugu zao wa nyumbani, jumla yao sasa ni 190, lengo kuu la nchi ni wafike 205 katika miaka mitatu ijayo, yaani kufikia mwaka 2023.

Mtaalamu huyo wa wanyamapori, anafafanua mchakato wa kuzaliana kwamba mimba ya faru inachukua kati ya miezi 15 na 16. Kwa lugha rahisi, ni wastani wa mwaka mmoja na robo.

**WALIVYOTOWEKA**

Ngoti anasema asilimia 90 ya faru walipotea duniani mwishoni mwa miaka ya 1990 kutokana na ujangili.

Ofisa huyo wa TANAPA anabainisha kwamba miaka ya 1970, Tanzania ilikuwa na faru 10,000, ikiwa nchi yenye faru wengi zaidi duniani, lakini idadi yao ilipungua hadi kufika 15 tu (asilimia 0.15) miaka ya 1990, hivyo kutoa hadhari ya tishio la kutoweka kabisa kwa wanyama hao.

Anasema mikakati iliyochukuliwa imesaidia kuongeza idadi hiyo, akiweka wazi kuwa mwaka 2018, nchi ilikuwa na faru 161 na mwaka huu wamefikia 190, likiwa ni ongezeko la faru 28 ndani ya miaka miwili.

"Hadi Machi mwaka huu, kulikuwa na faru 190 katika Hifadhi ya Taifa Mkomazi na Great Serengeti Ecosystem (mfumo wa ikolojia)," Ngoti anabainisha.

Ofisa huyo anaainisha ukanda huo wa ikolojia unajumuisha Hifadhi ya Taifa Serengeti, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, mapori ya Ikorongo, Maswa na Hifadhi ya Taifa ya Masai Mara iliyoko Kenya.

Anasema kuwa kutokana na kuimarishwa kwa ulinzi kwenye hifadhi za taifa, mwaka huu hakuna faru aliyepigwa na majangili.

**'BIBI' FARU FAUSTA**

Ngoti anabainisha kwamba mwaka jana alikufa faru mmoja nchini, aliyekuwa na upekee wake kuanzia jina la 'ubatizo' la Faru Fausta, aliyeaminika ndiye mzee zaidi duniani.

Faru Fausta alikufa tarehe kama ya leo mwaka jana kwenye Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro akiwa na umri wa miaka 57.

Kabla ya kifo chake, faru huyo jike alikuwa chini ya uangalizi maalum kwa kipindi cha miaka mitatu kutokana na afya yake kudhoofika na kuanza kushambuliwa na wanyama wakali mwituni.

"Faru Fausta kwa mara ya kwanza alionekana katika eneo la Ngorongoro mnamo mwaka 1965 na mwanasayansi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), akiwa na umri wa kati ya miaka mitatu na minne.

"Ilipofika mwaka 2016, afya yake ilianza kudhoofika. Wanyama wakali hususani fisi walianza kumshambulia na akapata vidonda vikubwa sana. Ilibidi tumtoe porini na kumweka kwenye uangalizi maalum.

"Vidonda vyake vilipona lakini afya yake bado ilikuwa dhoofu, hivyo hatukumrejesha porini," alisimulia Dk. Freddy Manongi, Mhifadhi Mkuu wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, katika taarifa ya kifo cha Faru Fausta.

Mnyama huyo alishika hadhi ya kitaifa, kwa kuwa mwaka 2017 suala la matunzo yake lilifikia hatua ya kuibua mjadala kisiasa ndani ya Bunge, mada kuu katika hoja zote zilibeba mtazamo wa msimamo wa maslahi yake.

**NINI KINACHOFUATA?**

Ngoti anasema mpango uliopo sasa ni kuwatawanya ndugu wa Faru Fausta katika makazi mapya ndani ya hifadhi za taifa za Burigi-Chato na Arusha.


Ofisa huyo wa TANAPA anabainisha kwamba, faru sasa wanalindwa kwa kifaa maalum cha kufuatilia mienendo yao na taarifa zao kupokewa kwenye vituo mbalimbali kwa teknolojia ya kisasa.

"Pembe za wanyama hawa huuzwa China na Vietnam ambako hutengeneza dawa za kienyeji zinazoaminiwa zinatibu homa, kupooza, saratani na kuongeza nguvu za kiume.

"Kwa Vietnam, mtu kuwa na jambia au kifaa kilichotengenezwa kwa pembe ya ndovu, ni ufahari mkubwa ndiyo maana watu wa huko hutoa fedha nyingi ili kupata kiungo hicho.

"Kwa sasa ujangili umepungua, kulikuwa na vigogo wa ndani ya serikali walishirikiana na watu wa nje kuangamiza wanyama hawa.

"Mkakati uliopo sasa ni kusafi-



Faru Fausta akiwa kwenye eneo maalum alilowekwa kwenye Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro enzi za uhai wake. Leo umetimu mwaka mmoja tangu kifo chake.

**Inaendelea Uk. 5**

RIPOTI MAALUM

# Ujangili ulivyowanyofoa faru 10,000 wakabaki 15

Inatoka Uk. 4

sha ndani na ndiyo maana tumeleta jeshi la uhifadhi na misitu," Ngoti anafafanua.

**UTASHI WA KISERIKALI**

Kamishna Msaidizi wa TANAPA, Godwell Meing'ataki, anasema hatua zinazoendelea kuchukuliwa kiserikali hadi sasa, zimekuwa msaada mkubwa katika kupunguza ujangili.


Anasimulia kuwa miaka ya nyuma, wahifadhi walijikuta kwenye matatizo makubwa walipotaka kuchukua hatua dhidi ya vitendo vya ujangili.

Kamishna Meing'ataki anasifu hatua kali za kiserikali zinazotawala kukabili nyendo zote za ujangili, ikiwamo watuhumiwa kuingizwa katika mkondo wa kisheria na kuwajibishwa ipasavyo.

"Huko nyuma unakamata mtuhumiwa, anakwenda polisi anaachiwa na unapata mashinikizo mengi kutoka kwa wakubwa na wakati mwingine inakugharimu wewe uliyekamata jangili.

"Kwa sasa, hata kesi zikienda mahakamani, hatua zinachukuliwa. Nyuma kesi nyingi zilisota mahakamani kwa muda mrefu na ziliishia kutupwa na majangili waliachiwa. Kwa sasa watu wanafungwa sana, ndiyo maana ujangili umepungua," anasema.

Kamishna Meing'ataki pia anarejesha sifa nyumbani kwamba kuongezeka kwa faru kunatokana na jitihada zao TANAPA, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA), Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro na Mamlaka ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI).




Hali ya ujangili ilivyo katika hifadhi za taifa. CHANZO: TANAPA Desemba 10, 2020.

**UFUNGUO**

**A: Hifadhi za taifa zilizo katika hatari zaidi ya ujangili**

**B: Hifadhi za taifa zilizo katika hatari ya ujangili**

**C: Hifadhi za taifa ambazo hazina ujangili**

**JESHI LINAVYOWAJIBIKA**

John Nyamhanga, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi wa TANAPA, anasema kuanzishwa kwa Jeshi la Uhifadhi, kumesaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza vitendo vya ujangili nchini.

Anasema jeshi hilo sasa limepewa mamlaka kisheria kushughulika na wahalifu hifadhini, akiisifu pia serikali kwa kuliwezesha jeshi hilo kwa silaha za kijeshi, mafunzo na teknolojia ya kisasa kukabiliana na wahalifu.

Jeshi hilo lililoanzishwa muda mfupi baada ya serikali ya awamu ya tano kuingia madarakani, lilizinduliwa rasmi na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, Novemba 17, 2018.

Kamishna Nyamhanga anabainisha kuwa tangu kuanzishwa kwa jeshi hilo, tayari watumishi wa TANAPA 2,871 kati ya 3,003, sawa na asilimia 96, wameshapitia mafunzo ya mabadiliko ya mfumo huo wa kijeshi.

Anasema kuwa kisheria, jeshi hilo sasa linawajibika kukusanya habari za kiintelijensia ndani na nje ya hifadhi, kuzuia, kukamata, kuweka kizuizini, kufanya upekuzi na upelelezi.

Mhifadhi huyo anasema jeshi lao limebaini ujangili umechukua mwelekeo mpya wa matumizi ya silaha za kisasa, mbinu za kijeshi na ongezeko la wimbi la mitandao ya kijangili ya kitaifa na kimataifa pamoja na matumizi ya fedha haramu.

Kamishna Nyamhanga anabainisha kuwa, katika kipindi cha miaka minne (2015/16 hadi 2018/19), Jeshi la Uhifadhi lilikamata majangili 11,838 na maelfu ya silaha za moto, zikiwamo za kivita.

**KIKWAZO KIPYA**

Kamishna Nyamhanga anasema kuwa, jeshi lao pia limebaini baadhi ya hifadhi za taifa na mapori ya akiba yanakabiliwa na tatizo la kuongezeka kwa matukio ya ugaidi kutokana na baadhi ya maeneo yake kugeuzwa makambi ya maficho ya makundi ya magaidi.

Anasema hali hiyo si tu kwamba inatishia uhifadhi, bali pia inahatarisha usalama wa nchi, akiitaka jamii inayoishi karibu na maeneo ya hifadhi kutoa taarifa kwa mamlaka ili kukabiliana na makundi hayo.

"Tatizo hili pia tunalishughulikia kwa kuimarisha doria na kukiongeza nguvu kitengo chetu cha intelijensia," Kamishna Nyamhanga anasema.

**MIKAKATI YA WIZARA**

Akizungumzia tatizo la ujangili, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Allan Kijazi, anasema mikakati ya kiserikali imesaidia kupunguza wimbi la ujangili nchini.

Hata hivyo, Dk. Kijazi anadokeza kuwapo kwa dalili za kuibuka wimbi jipya la ujangili wa wanyamapori walio hatarini kutoweka, wakiwamo tembo na faru, likihusisha kuwajenga imani wananchi kwamba maini na mafuta ya wanyama hao yanasaidia kuponya saratani ya ini, kizazi kwa kinamama na vidonda vya tumbo.

Anasema majangili wametumia udanganyifu huo kuaminisha watu kuwa wakitumia maini na mafuta ya wanyama hao, watapona saratani ya ini na kizazi pamoja na vidonda vya tumbo, jambo ambalo anasisitiza kuwa halina ukweli.

Anasema wamebaini kwamba, kutokana na ushawishi huo, baadhi ya wananchi wameanza kutumia mbinu za kuweka sumu kwenye maboga na misumari kwenye maeneo wanayopita tembo ili kupata maini na mafuta ya wanyama hao.

"Wanapowaua tembo hao, wanaofanya kampeni hizo wananunua meno ya tembo. Nitoe rai kwa wananchi kwamba hakuna ushahidi wote wa kitaalamu unaoonesha maini na mafuta ya tembo yanatibu magonjwa hayo.

"Hizo ni mbinu zinazotumika kuwadanganya wananchi ili wawatumie kufanikisha biashara ya meno ya tembo. Hatutasita kumchukulia hatua mwananchi yeyote bila kujali uwezo wake au nafasi yake katika jamii," Dk. Kijazi anaonya.

Vilevile, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi wa TANAPA (Idara ya Mawasiliano), Paschal Shelutete, anasema shirika lao limeweka mikakati kutimiza malengo ya serikali kudhibiti ujangili wa wanyampori na misitu.

Anasema mikakati hiyo inajumuisha kuimarisha ulinzi wa wanyamapori na kutatua migogoro baina ya wananchi na hifadhi, ili wananchi washiriki kulinda hifadhi na kufichua majangili.

| MWAKA | SMG | RIFFLE | SHOTGUN | GOBOLE | MAJANGILI |
|---|---|---|---|---|---|
| 2015/16 | 64 | 125 | 126 | 1,006 | 3,848 |
| 2016/17 | 16 | 64 | 21 | 115 | 4,455 |
| 2017/18 | 2 | 6 | 1 | 54 | 2,246 |
| 2018/19 | 35 | 5 | 2 | 10 | 1,399 |
| JUMLA | 117 | 200 | 150 | 1,185 | 11,838 |

Silaha na majangili waliokamatwa na Jeshi la Uhifadhi kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2018/19. CHANZO: TANAPA Desemba 10, 2020.

**UHIFADHI TANZANIA**

Sera ya Wanyamapori ya Tanzania (2007) inabainisha kuwa historia ya uhifadhi wa wanyamapori nchini ilianzia mwaka 1891, yaani miaka 129 iliyopita.

Hiyo ilikuja kama matokeo ya kuzaliwa kwa sheria za kudhibiti uwindaji zilizoanzishwa na utawala wa Kijerumani uliokuwapo katika zama hizo.

Kwa kurejea sera iliyopo sasa, sheria hizo za awali zililenga kudhibiti uvunaji holela wa wanyamapori; kuhakiki mbinu za uwindaji na biashara ya wanyamapori waliokuwa hatarini kutoweka.

Hifadhi ya kwanza ya wanyamapori nchini ilianzishwa na Wajerumani hao miaka 14 baada ya kutunga sheria katika ukanda wa hifadhi maarufu ya sasa iitwayo Pori la Akiba Selous, mwaka 1905.

Sera inafafanua kwamba kanuni za kitaalamu zilizotumika kuteua maeneo ya hifadhi za wanyamapori, zilizingatia vigezo kama kuwapo wanyama wakubwa pekee na siyo mengine ya ziada yanayotawala sasa, kama makundi yao ya baionuai za kibaiolojia.

Baada ya kupita miaka 16 ya hifadhi kuanzishwa, Tanganyika ikiwa chini ya utawala wa mkoloni mpya, Uingereza, mwaka 1921, kukaanzisha Idara ya Wanyamapori sambamba na mwaka mmoja baadaye, serikali ililitangaza rasmi Pori la Akiba Selous.

Sera inafafanua kuwapo historia ya ushuhuda wa hifadhi nyingine mbili kuanzishwa miaka sita baada ya hatua ya mwisho mwaka 1922.

Hapo panatajwa iliyokuwa Bonde Kuu Funge la Ngorongoro (sasa Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro) na Pori la Akiba Serengeti (sasa Hifadhi ya Taifa Serengeti).

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jamii ibadilike na kusimama imara katika malezi ya watoto

**WAUMINI** wa madhehebu ya Kikristo nchini, juzi waliungana na Wakristo wenzao duniani kuadhimisha Sikukuu ya Krismasi, ikiwa ni kumbukumbu ya kuzaliwa kwa Mwokozi Yesu Kristo zaidi ya miaka 2,000 iliyopita.

Katika kusherehekea sikukuu hiyo kubwa, waumini hao walikusanyika katika nyumba za ibada kuanzia usiku wa mkesha na baadaye ibada zilizofanyika jana, huku ibada ya kitaifa ikifanyika katika Kanisa la Biblia, Mtwara.

Maaskofu na wachungaji walioongoza ibada hizo, walisisitiza mambo mbalimbali ambayo ni ya muhimu kwa ustawi wa jamii ya Watanzania na taifa kwa ujumla.

Miongoni mwa mambo hayo ni matumizi ya bidhaa za ndani kwa ajili ya viwanda, mwafaka uliosababisha kuanzishwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK), mauaji ya vikongwe, kurekebishwa kwa baadhi ya kasoro zilizojitokeza katika uchaguzi mkuu uliopita na kumshukuru Mungu kutokana na kuiponya Tanzania dhidi ya maradhi ya corona, janga ambalo bado linaisumbua dunia kwa sasa.

Licha ya kuzungumzia mambo hayo na mengine, baadhi ya maaskofu walijikita zaidi katika malezi ya familia ambayo yamekuwa sehemu ya matatizo yanayoikabili jamii Tanzania, Afrika na dunia nzima kwa sasa.

Maaskofu hao, katika mahubiri yao, waliweka bayana kwamba jamii inapaswa kusimama kidete katika suala la malezi, ili kuepusha mmomonyoko wa maadili, unyanyasaji na ukatili wa kijinsia na ongezeko la watoto wa mitaani.

Katika kubainisha hilo, walisema kumekuwa na vitendo vya ubakaji na na ukatili wa kijinsia ambavyo vimelitia doa taifa, huku wakisema miongoni mwa watu wanaoshiriki vitendo hivyo ni Wakristo.

Askofu Mkuu wa Kanisa la Biblia Tanzania, John Mchopa, katika mahubiri ya Krismasi kwenye ibada ya kitaifa iliyofanyika Mtwara, alisema jamii haina budi kurejea mafundisho ya neno la Mungu katika kuwalea watoto katika maadili mema na njia ziwapasazo.

Mkuu huyo alisema kukosekana kwa malezi mema kunasababishwa kwa kiasi kikubwa na migogoro ya kifamilia, kumesababisha ukatili dhidi ya watoto, mifarakano, kuyumba na kuvunjika kwa ndoa pamoja na ongezeko la watoto wa mitaani.

Licha ya visababishi hivyo, kiongozi mwingine wa kiroho alisema kukosekana kwa malezi bora ndani ya familia kunatokana na idadi kubwa ya wazazi kutumia muda mwingi kwa ajili ya kazi, starehe na kutumia simu kwa muda mrefu, huku wakilipa kisogo suala la malezi ya watoto.


Ni ukweli usiopingika kwamba jamii inapaswa kurejea katika wajibu wake juu ya malezi ya watoto, ili kujenga jamii na taifa lenye maadili mema. Katika kufanya hivyo, kila mtu anapaswa kusimama katika nafasi na zamu yake katika suala zima la malezi ya watoto.

Kwa kufanya hivyo, jamii inapaswa kutambua kuwa itawandaa watoto katika uongozi na maendeleo ya taifa la kesho katika nyanja mbalimbali na kuwaepusha dhidi ya vitendo viovu kama vile rushwa na ufisadi pindi wanapopewa majukumu ya uongozi katika nafasi mbalimbali.

Pia ikumbukwe kwamba taifa lenye watoto waliolelewa katika misingi imara litatoa viongozi wenye maadili mema na wanaojitambua ambao watakuwa wazalendo kwa kweli kwa taifa lao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Ukiona mapovu katika haja ndogo chukua hatua mapema

**KILA** magonjwa yana dalili ambazo ni muhimu kuzifahamu na kuchukua hatua za kwenda kufanya vipimo pale zinapojitokeza, ili kupata matibabu haraka iwezekanavyo, kuepuka kuhatarisha afya.

Mfano mmojawapo ni dalili za magonjwa ya figo zinazoelezwa kuwa hutofautiana kutoka mtu mmoja na mwingine, na hutegemea zaidi na ugonjwa uliopo na ukali wake na dalili huwa za jumla na zisizodhihirika vyema.

Kuvimba uso, miguu na tumbo, ni miongoni mwa dalili za kawaida za ugonjwa wa figo ingawa ni muhimu kuelewa kuwa kuvimba si lazima iwe ni figo kushindwa kufanya kazi.

Dalili nyingine ni kukosa hamu ya chakula, kusikia ladha isiyo ya kawaida mdomoni na kushindwa kula chakula vyema. Dalili hizo zinatajwa kuwa ni shida za kawaida zinazopatikana kwa watu wenye tatizo la figo.

Lakini kwa wagonjwa wa kushindwa kwa figo kufanya kazi kuwa na shinikizo la damu ni kawaida, na iwapo shinikizo hilo linatokea chini ya umri wa miaka 30 au liko juu wakati wa uchunguzi, sababu itakuwa ni figo.

Kimsingi, ziko dalili zingine za figo zinazoelezwa na wataalamu wa afya ikiwamo ya kuwa na mapovu mengi kwenye haja ndogo, ambayo huenda baadhi ya watu wanaweza wasiijue.

Wanaweza wasiijue au wasiwe nayo makini kwa sababu haja ndogo kuwa na mapovu ni jambo la kawaida, hivyo hata yakiongezeka inawezekana mtu asitambue kwa kuwa amezoea kuona mapovu.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani ya Mwili wa Binadamu kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dk. Lucas Nzobendo, anabainisha kuwa mtu akiona mapovu mengi katika haja ndogo ashtuke na kuchukua hatua.

Anakiri kwamba kwa kawaida haja ndogo ina mapovu, lakini si mengi na haihitaji kipimo kutambua wingi wa mapovu bali mtu mwenyewe anaweza akagundua kuwa mapovu hayo si ya kawaida.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, mtu anapotoa mapovu mengi katika haja ndogo, ni moja ya dalili za kuwa ana tatizo, figo inashindwa kufanya kazi vizuri na kutoa nje vitu visivyotakiwa kutoka.

Hali hiyo ya haja ndogo kuwa na mapovu inaweza kuwafanya watu wasigundue kuwa wana tatizo, hivyo anashauri watu kujichunguza mara kwa mara wanapokwenda haja ndogo, ili kubaini kama mapovu ni mengi au la.

Kutokana na maelezo hayo ya mtaalamu wa afya, Muungwana anaamini kuwa, ingawa baadhi ya watu hawana kawaida ya kupima afya, lakini wanaweza kujichunguza wenyewe ili kutambua baadhi ya dalili za magonjwa.

Msisitizo wake ni kwamba, haja ndogo kuwa mapovu, inaweza kuwa ishara ya matatizo ya figo au protini zilizozidi mwilini, hivyo suala la kuchunguza afya ni la msingi ili kubaini kuna nini.

Kama wasemavyo wataalamu wa afya, mwili una mifumo mbalimbali ambayo hushirikiana kwa karibu katika ufanyaji kazi, na linapotokea tatizo katika mfumo fulani huonekana kwenye mabadiliko kadhaa ya kimwili.

Ni muhimu kila mtu achukulie kwa uzito suala la mapovu mengi kwenye haja ndogo, badala ya kuzoea tu kwamba kwa kawaida huwa ina mapovu na kuacha tatizo likiendelea kukua.

Figo ni miongoni mwa viungo muhimu katika mwili binadamu, ambacho wataalamu wa afya wanasema, kina kazi ya kudhibiti na kuhifadhi virutubishi na maji na kuondoa mabaki kupitia haja ndogo.

Kiungo hicho pia kinaelezwa kuwa, kinachuja damu, ili kuondoa sumu mwilini kwa lengo la kuhakikisha mtu anakuwa na afya salama, hivyo jambo la msingi ni kila mmoja ahakikishe anajua dalili zote za kuwa tatizo katika figo.

Kimsingi, wataalamu wa afya wanasisitiza umuhimu wa kuchunguza afya kila mara kama njia mojawapo na kumfanya mtu kuwa salama zaidi badala ya kusubiri hali kuwa mbaya ndipo achukue hatua.

## SAFU

### FIKRA MBADALA

# Tunamaliza na tunaanza mwaka 2021 bila Mzee Mkapa



Nkwazi Mhango, Canada

**Mmojawapo alijifanya kuzungusha akisema "siamini aliyeandika tanzia hii ni wewe. Maana Kiingereza kimepwaya tena broken." Nilicheka na nikamjibu bila hasira kuwa: kwanza, Kiingereza siyo lugha yangu.**

KWANZA, kwa kipekee zaidi, tutume safari na heri za Noeli na Mwaka Mpya 2021 kwa wapenzi wote wa safu hii pia tuwaalike katika kumkumbuka mzee wetu Benjamin William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu aliyetutoka tarehe 24 Julai, 2020.

Kifo cha mzee Mkapa kilitokea wakati safu hii haijarejea hewani. Tunaomba kufunga mwaka huu kwa; mosi, kutoa salamu za rambirambi kwa taifa na familia. Pili, kama kumbukizi la mzee Mkapa, safu hii leo imeamua kudurusu namna atakavyokoswa hasa mwaka 2021 tunaotegemea kuanza siku chache zijazo inshallah.

Kwa tuliomfahamu mzee Mkapa kama gwiji la diplomasia na usuluhishi, kifo chake si pigo kwetu tu bali kwa nyanja ya diplomasia na usuluhishi Afrika na duniani kote. Binafsi, mzee Mkapa alinisaidia mawazo wakati naanza kusomea shahada yangu ya uzamivu (PhD) kwenye masuala ya amani na migogoro pale nilipomwomba anipe uzoefu wake.

Hii ni baada ya rafiki na ndugu yangu mzee Pius Msekwa sasa 'Daktari', aliyetunukiwa shahada hii ya heshima hivi karibuni kunipa barua pepe yake. Nilimwandikia kumweleza shida zangu. Naye, bila kusita, alijibu "Bwana Mhango, naomba unipe muda kidogo kwani sijisikii vizuri."

Kusema ukweli majibu yake ya kiungwana na kinyenyekevu yalinipumbaza ukiachia mbali kutoa mawazo yake tena yenye kujibu maswali mengi na marefu ya kitaaluma bila kuacha kuniambia kuwa nikihitaji zaidi nisisite kumweleza.

Alinipa moyo kusoma ili baadaye niitumie elimu yangu kwa faida yangu na taifa jambo ambalo licha ya kufanya nimkumbuke, sitalisahau.

Kutokana na namna nilivyowasiliana na mzee Mkapa, tena kwa kujibu yeye mwenyewe na si wasaidizi wake, nilipoandika tanzia ya kifo chake, wapo hasa mahasidi na wakosoaji wake walionitumia salamu binafsi kusema kuwa ima sikumjua mzee Mkapa au niliamua kumpendelea na kumpamba.

Mmojawapo alijifanya kuzungusha akisema "siamini aliyeandika tanzia hii ni wewe. Maana Kiingereza kimepwaya tena broken." Nilicheka na nikamjibu bila hasira kuwa: kwanza, Kiingereza siyo lugha yangu. Na pili kuwa ni hicho hicho kilichopwaya na broken ndicho kilichoniwezesha kukubaliwa kusoma shahada ya uzamivu tena kwenye nchi inayotumia Kiingereza kama lugha yake ya kwanza ukiachia mbali kuandika vitabu zaidi ya 20 vya kitaaluma kwa lugha hii hii.

Ni bahati mbaya ujumbe ulifika na mhusika hakunijibu tena. Maskini huyu jamaa ambaye ananizidi kiumiri ila si kitaaluma pia namheshimu hakujua kuwa mzee Mkapa alikijua Kiingereza kama alivyo mzee Msekwa, lakini hawakuwahi kuniambia kuwa Kiingereza changu ni cha kuungaunga.

Hata kitabu cha Magufulification, the Concept that Will Define the Future of Africa and the Man who Makes Things Happen, nilichoandika na mzee Msekwa ukiachia kitabu kizima cha tenzi za kimombo kiitwacho Kudos to President Magufuli, mbali kazi nyingine ambazo mzee Msekwa amenishirikisha zote za kimombo na hakuwahi kulalamikia kizungu changu.

Kwa vile mimi ni Mtanzania, kama Mkapa, pamoja na kujua kimombo, bado najivunia lugha yangu ya taifa ya Kiswahili. Mwingine nilimwambia kuwa mzee Mkapa, sawa nawe na nami, alikuwa na upungufu wake kama binadamu, ila mazuri yake yalishinda mabaya yake. Nilimwambia kuwa asiye na dhambi awe wa kwanza kumtupia mawe mzee Mkapa tena akiwa marehemu kama yeye ataishi milele.

Ni kweli mzee Mkapa wapo aliowakwaza. Wamesamehewa akina Idi Amin itakuwa yeye? Juzi juzi nilikuwa nawasiliana na ndugu Madaraka Nyerere juu ya upatanisho wa marehemu baba yake (Baba wa Taifa). Na alikuwa na moyo mkunjufu kunitambulisha kwa Jaffar Amin (mtoto wa Amin) kuhusiana na harakati zao za kuzidi kuleta Tanzania na Uganda karibu.

Tuache chuki na utani. Mzee Mkapa, ni mtu aliyeutumikia umma kwa maisha yake yote tena kwa moyo mmoja na mkunjufu. Pia hakuwa mgeni kwa Watanzania na hata kimataifa.

Burundi bado wanamkumbuka kwa mchango wake katika kuleta amani kwenye taifa hilo ambalo lilipata utulivu baada ya Mkapa kuwasuluhisha. Uganda hawatasahau alivyowasaidia kuunda serikali baada ya kuangushwa kwa Idi Amin.

Pia mzee Mkapa alisifika kwa ujasiri wake na wakati mwingine ubabe kidogo pale alipoudhiwa. Hata hivyo, alikuwa mtu mnyenyekevu, msomi na muwazi.

Rejea sera yake ya 'Uwazi na Ukweli' iliyowasilisha falsafa yake kiutawala. Hata hivyo, mzee Mkapa hakuwa malaika. Pamoja na hii, ni mmojawapo wa viongozi waliokiri upungufu wake na utawala wake pale alipoandika wazi wazi kwenye kitabu cha maisha yake cha My Life, My Purpose A Tanzanian President Remembers kilichotoka mwaka mmoja kabla ya kufikwa mauti. Katika kitabu hiki, Mkapa alikiri wazi wazi kuwa kulikuwa na upungufu katika baadhi ya sera zake kama vile uwekezaji ambao ulizua manung'uniko kwa baadhi ya Watanzania.

Kitendo chake cha kukiri tena wazi wazi kwa maandishi kinamweka kwenye daraja la juu la viongozi waadilifu. Maana Walatin husema verba volant, scripta est manent est, yaani maneno huupaa, lililoandikwa ni la milele.

Tumalizie kwa kumkumbuka marehemu mzee Benjamin Wiliam Mkapa (Mungu ampe pumziko jema peponi). Hakika mwaka ujao utakuwa na pengo kutokana na kifo cha mzee Mkapa. Lala Mahali Pema Peponi Mzee Benjamin William Mkapa. Hamba Kahle Ubaba Mkapa.

### MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Tuwe na magulio salama au hatarishi?



Na Joseph Kulangwa

**Kuna maeneo ambako kwa siku moja ya wiki, mtaa au mitaa hufungwa na kutumiwa kwa magulio ambako watu wengi hujitokeza kununua bidhaa, zikiwamo nguo na vyakula na kupunguza gharama za kusafiri kufuata huduma hizo masokoni ambako huhitaji nauli.**

KAMA kuna jambo linamnyima usingizi Rais John Magufuli, ni hili la wanyonge kunyimwa haki. La wanyonge kunyimwa fursa zilizopo, za kujikwamua kiuchumi.

Tangu aingie madarakani mwaka 2015, Rais Magufuli alisisitiza watu wa hali ya chini kutonyanyaswa, akishinikiza wafanyabiashara ndogo mijiniwamachinga, kuachwa wafanye shughuli zao bila dhahama.

Kama hiyo haitoshi, hatimaye akaona kama anachokisema pengine hakieleweki, akaamua kuwatengenezea vitambulisho maalumu, ambavyo hivi sasa vinaboreshwa ili wavitumie kwa fursa zaidi.

Alitoa pia maelekezo ya kuondolewa kwa tozo mbalimbali walizokuwa wakitozwa wakulima vijijini, hasa walipokuwa wakisafirisha mazao yao ya chakula, huku akisisitiza kwa kauli ya "wakati analima hukumsaidia, iweje anavuna unamfuata kumkandamiza kwa kodi!"

Wengi wanaomwelewa anachokitaka, hawatamsahau kwa hatua alizochukua, kuhakikisha mnyonge analindwa na ananufaika na jasho lake bila kunyonywa na mwenye nguvu. Hakika ni jambo la kujivunia na kupewa kongole.

Lakini kuna nyakati nia hii njema ya Rais, inatiwa mchanga, ama na wamachinga wenyewe, au wanaowasimamia kwa maana ya serikali za mitaa, ambazo zinajisahau na kuwafanya kujiamulia hata mambo yasiyostahili.

Mathalan, katika kuhakikisha wafanyabiashara ndogo ndogo wanapata riziki zao bila matatizo, huku wananchi nao wakipata huduma hizo kwa wafanyabiashara hao, kuna magulio yameanzishwa katika baadhi ya maeneo Dar es Salaam.

Kuna maeneo ambako kwa siku moja ya wiki, mtaa au mitaa hufungwa na kutumiwa kwa magulio ambako watu wengi hujitokeza kununua bidhaa, zikiwamo nguo na vyakula na kupunguza gharama za kusafiri kufuata huduma hizo masokoni ambako huhitaji nauli.

Lakini katika baadhi ya magulio kumekuwa na adha ambayo inaweza kuepukika, ingawa kwa bahati mbaya, wasimamizi hata wanapoambiwa huziba macho na masikio, wakichelea kuudhi wafanyabiashara wao.

Magulio yanafanyika mitaani, pembeni mwa makazi ya watu. Idadi kubwa ya wafanyabiashara hujitokeza kupanga bidhaa zao mezani, kuning'iniza mitini na hata kupanga chini kutokana na ufinyu wa maeneo.

Lakini idadi kubwa hiyo ya wauzaji na wanunuzi, hukosa mahali pa kujisitiri kwa haja kubwa na ndogo, kwa sababu hakuna vyoo. Hukosa pia mahali pa kutupa takataka zitokanazo na shughuli hizo, kwa kuwa hakuna vifaa au maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo.

Kwa kuwa ni maeneo ya mitaa na makazi ya watu, si rahisi kwa vyoo kuchimbwa kwa ajili ya siku hiyo moja ya wiki. Matokeo yake, wadau wa magulio hayo, kwa maana ya wanunuzi na wauzaji, hujisaidia haja ndogo kwenye chupa za plastiki na kuzitupa, hususan nyakati za usiku.

Matokeo yake, watoto wanaocheza mitaani, huokota chupa zenye haja ndogo wengine wakidhani ni juisi zilizotupwa na kuzibugia, maskini bila hata kujua madhara yake, ambayo hakuna asiyeyafahamu.

Halikadhalika, baadhi ya watu wasio na nia njema, hutumia fursa hiyo ya usiku kudokoa mali zilizo katika makazi yasiyo na uzio, na kusababisha hasara kwa wamiliki, na hiyo inatokana na kwamba hata magulio yenyewe hayana ulinzi.

Si kwamba viongozi wa mitaa hawajui adha hiyo, walishaambiwa, lakini katika muktadha uleule wa kutotaka kuudhi wadau, wananyamaza na hali inaendelea kuwa mbaya. Ikumbukwe wafanyabiashara hao na hata wanunuzi, ndio wapigakura.

Tujiulize, je, tutakuwa na wapigakura hao kama watadhurika na tabia inayoendelea katika magulio hayo? Je, kwa hali hiyo na mazingira hayo, magulio hayo bado yanastahili kuendelea kuwapo?

Kama jibu la swali la pili ni ndiyo, basi utafutwe utaratibu wa kuwa na vyoo vya dharura, vifaa vya kuhifadhia taka, ili tusijelia kilio cha mbwa, tutakapokuwa tumevamiwa na magonjwa ya mlipuko na kuanza kutupiana lawama zisizo za msingi.

**Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Ni aibu viongozi mikoa, wilaya kusubiri maagizo kutoka juu



Na Thobias Mwanakatwe

**Waziri Mkuu katika kuweka msisitizo ili ujenzi wa vyumba ukamilike kwa wakati, aliwataka wakuu wa mikoa wasaidizi wao wasiende likizo ya Krismasi wala Mwaka Mpya hadi wahakikishe ujenzi wa vyumba vya madarasa unakamilika katika muda uliopangwa.**

BARAZA la Taifa la Mitihani Tanzania (NECTA), hivi karibuni lilitangaza matokeo ya mitihani ya darasa la saba iliyofanyika mwaka huu.

Siku chache baada ya NECTA kutangaza matokeo hayo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, alitangaza majina ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza mwakani.

Wakati akitangaza wanafunzi watakaojiunga na masomo ya kidato cha kwanza mwakani, Jafo alisema wanafunzi 759,706 sawa na asilimia 91.1 ya waliofaulu, wamechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza. Akasema kati ya hao waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza, wavulana ni 368,174 na wasichana ni 391,532.

Jafo akasema wanafunzi 74,166 sawa na asilimia 8.9 wakiwamo wavulana 34,861 na wasichana 39,305 hawakupangiwa shule katika awamu ya kwanza kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa.

Aliitaja mikoa ya Mwanza, Mtwara, Lindi, Katavi, Kagera, Njombe, Ruvuma, Songwe na Tabora kuwa imewapangia shule wanafunzi wote waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza kutokana na kuwa na vyumba vya madarasa vya kutosheleza wanafunzi wote waliochaguliwa.

Baadaye, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alitoa agizo kwa wakuu wa mikoa wote kuhakikisha wanasimamia ujenzi wa vyumba vya madarasa ili wanafunzi wote waliochaguliwa wajiunge na masomo ya sekondari.

Majaliwa alisema ifikapo Februari 28, mwakani, wanafunzi wote wawe wamekwenda sekondari wa awamu ya kwanza na ya pili na pia kuwapo na madawati na viti vya kutosha katika shule hizo.

Waziri Mkuu katika kuweka msisitizo ili ujenzi wa vyumba ukamilike kwa wakati, aliwataka wakuu wa mikoa wasaidizi wao wasiende likizo ya Krismasi wala Mwaka Mpya hadi wahakikishe ujenzi wa vyumba vya madarasa unakamilika katika muda uliopangwa.

Hii si mara ya kwanza kwa viongozi wa juu kutoa maagizo kwa wasaidizi wao kwenye ngazi za wilaya na mikoa kusimamia ujenzi wa vyumba vya madarasa na utengenezaji wa madawati kwa ajili ya shule za msingi na sekondari nchini.

Nakumbuka Rais John Magufuli alipoingia madarakani kwa mara ya kwanza, aliagiza wakuu wa mikoa kutengeneza madawati na kwamba ambaye mkoa wake utashindwa kukamilisha kazi hiyo katika muda aliokuwa ameutoa, atakuwa amejifukuzisha kazi.

Ninachohoji ni kwa nini wanafunzi washindwe kuanza masomo kwa wakati kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa ilihali kila mkoa unajua idadi ya watahiniwa wa darasa la saba, hivyo kujua mahitaji ya madarasa?

Wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi wa halmashauri tuseme wanakuwa hawajui mahitaji ya madarasa katika mikoa na wilaya zao hadi wasubiri maagizo ya viongozi wa juu ndipo waanze kukimbizana katika wakati ambao wanafunzi walipaswa kuanza masomo?

Tangu maagizo yametolewa na Waziri Mkuu, hivi sasa katika wilaya yamekuwa kama mashindano kwenye mitandao kila mtu kuweka picha aonekane anapambana kushiriki ujenzi wa vyumba vya madarasa kana kwamba jambo hili walikuwa hawalijui.

Ifike wakati wateule wa Rais wawe wabunifu na kuzitatua kero za wananchi kwenye maeneo yao badala ya kusubiri kusukumwa na viongozi wa juu wakati wanafahamu wajibu na majukumu yao.

Hata Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu tumekuwa tukishuhudia wanapofanya ziara mikoani, wananchi wanawasilisha kero ambazo zingeweza kupatiwa ufumbuzi na viongozi wa wilaya na mkoa. Lakini kwa sababu inaonekana wateule hao baadhi yao hawako makini wanashindwa kutatua changamoto za wananchi.

Wateule hawa wa Rais lazima watambue kwamba wamepewa nafasi hizo, ili wamsaidie Rais kutatua changamoto zinazowakabili wananchi kwa sababu Rais hawezi kufika kila wilaya, kata na kijiji lakini wao wanawajibika kuzitatua kero hizo.

Pia wateule hao lazima watambue kuwa nafasi walizopewa si kwamba wao ni bora au wana sifa kuliko wengine bali bahati imewaangukia wao tu, hivyo wanapaswa kuwajibika vizuri kutatua kero za wananchi na kumpunguzia mzigo mkubwa Rais.

Uzuri awamu hii ya pili ya serikali ya Rais Magufuli ameshaweka wazi kuwa wenye sifa na elimu ya kutosha ni wengi na kwamba waliowekwa akiba ni wengine kwa maana ukizingua anapachikwa mwingine.

Kutokana na suala la vyumba vya madarasa kuwa wimbo usioisha, ikifika mwaka 2022 wanafunzi wengine wakachaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza, huku kukiwa na uhaba wa madarasa, watakaokumbwa na tatizo hilo watumbuliwe kwa sababu watakuwa wameshindwa kutimiza wajibu wao.

Kimsingi, hata sisi wananchi wako tumechoka kukimbizana na wakuu wa mikoa na wilaya katika ujenzi wa vyumba vya madarasa hasa pale nyie viongozi wa juu mnapowapa maagizo dakika za majeruhi. Tuwajibike kuijenga Tanzania yetu.

Kwa maoni na ushauri tuwasiliane kwa barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com

## DARASA LA NDOA

# Uongozi wa familia wenye mafanikio -2



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka
0744000066

**Maisha ya baba na mkewe yawe mfano bora kwa watoto. Awe mwadilifu na mwajibikaji katika familia. Baba asipowajibika katika familia yake, anapoteza umuhimu wa uwapo wake na kushusha thamani yake katika familia.**

KATIKA sehemu ya kwanza ya makala hii, tuliangalia umuhimu wa uongozi bora katika familia pamoja na sifa, ili uongozi huo uonekane kuwa wenye mafanikio. Lakini niligusia kwamba ili kuwa na uongozi wenye mafanikio katika familia, mume anapaswa kuwa kiongozi bora wa familia kwa maneno na matendo.

Sambamba na hilo, nilisema mume ni lazima amfahamu mke wake na kutambua umuhimu wa uwapo wake katika familia. Pia mume na mke ni lazima waishi pamoja na kwa umoja. Kwa maneno mengine waishi na kufanya mambo kama timu na hii itasaidia kuwashinda maadui wa ndoa na familia.

Ili kuwa na uongozi wa familia wenye mafanikio, nilieleza kuwa ziko sifa nane muhimu katika kufanikisha hilo. Katika sifa hizo, wiki iliyopita niligusia sifa tatu ambazo ni kwanza, mume kumfahamu mke wake na kujua anachopenda. Pili, ni ushirikishwaji katika mambo mbalimbali ndani ya familia, na tatu, mawasiliano bora.

Katika mwendelezo wa sifa hizo, ili kuwa na uongozi wenye mafanikio, baba ni lazima awe mfano na kielelezo kizuri kwa familia yake. Baba awe mfano kwa kauli, mwenendo na matendo yake kwa familia yake.

Maisha ya baba na mkewe yawe mfano bora kwa watoto. Awe mwadilifu na mwajibikaji katika familia. Baba asipowajibika katika familia yake, anapoteza umuhimu wa uwapo wake na kushusha thamani yake katika familia.

**KUTOA MIONGOZO, MAELEKEZO NA MAAMUZI YENYE TIJA KWA WAKATI**

Baba ni mjenzi wa nidhamu ya familia. Wababa watengeneze mfumo wa maisha ya familia zao na wawe na macho yenye kuona mbali kuhusu mahitaji ya familia (mf. uwekaji akiba, kuandaa wosia, nk).

Uwapo mgawanyo wa majukumu katika familia na kugawa madaraka na majukumu kwa makini, ni jambo muhimu kwani si lazima kila jambo lifanywe na baba. Kuna mambo ya kufanywa na mama na mengine ya kufanywa na watoto. Baba anapotaka kufanya kila kitu mwenyewe, anakaribisha msongo mkubwa wa mawazo na kifo.

**KUTAMBUA VIPAWA, UWEZO WA MKE**

Mungu hakukusudia mume na mke waishi kwa mashindano bali kwa kukamilishana. Kiongozi mzuri hujali vipawa na uwezo wa wale anaowaongoza. Hivyo, mume mwenye kujali atatambua vipawa na uwezo wa mke wake. Atamtia moyo mke wake inavyopaswa na kumsaidia. Ifahamike kuwa wanawake hupenda mwanamume anayejali hisia zao na maendeleo yao.

**UKARIBU NA FAMILIA**

Muda mwingi katika maisha yetu tunautumia katika kazi zetu kuliko familia zetu. Ni muhimu kufanya kazi kwa ajili ya maisha. Hata hivyo, tunahitaji muda wa kazi na muda wa familia. Mara nyingi kazi zimetuweka mbali na familia zetu, hivyo kushusha hadhi ya utu wetu.

Familia nyingi zimekosa kufurahia uwapo wa baba kwa sababu ya muda mwingi baba kutokupatikana nyumbani.

Hali kadhalika, katika ndoa nyingi, unakuta mke anakosa kufurahia uwapo wa mume wake.

Mahali pengine, watoto nao wanapoteza pendo na baba yao. Wengine wamechukia hata kazi za baba zao. Hali hii imesababisha wakati wakiwa watu wazima, thamani yao wanaelekeza kwa mama zaidi kuliko baba yao kwa sababu mama ndiye aliyekuwa na muda nao, jambo ambalo limesababisha migogoro ya kifamilia.

Hali kadhalika, mama anapokosa muda na familia yake, hali kama hiyo hujitokeza kwa mume na watoto pia.

Wababa wengi, wakiisha kuleta mahitaji ya nyumbani wanaona wamemaliza. Ni muhimu ikafahamika kuwa, kutunza familia ni zaidi ya kutoa mahitaji ya nyumbani. Familia inamhitaji baba kuliko vitu. Ukaribu wa baba kwa familia yake ni muhimu sana kuliko vitu.

**KUWAJIBIKA KWA MAKOSA YAKE**

Kuwa kiongozi haimaanishi kutokufanya makosa. Kiongozi ni mwanadamu anayeweza kukosea. Baba kama kongozi wa familia anaweza kukosea vile vile kwani kama wanadamu hatuwezi kuwa sahihi siku zote.

Kwa msingi huu, ni muhimu baba akitambua makosa yake awe mwepesi kujikosoa na kujisahihisha. Ni muhimu baba awe muwazi kwa watoto wake kama kuna makosa aliyoyafanya wakati wa ujana wake, awaeleze watoto wake ili watoto wasiyafanye wakati wao, kwani yatawaharibu.

**■Dk. Mlyuka ni Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishughulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi ya watoto.**

**Kwa maoni na ushauri, wasiliana naye kwa baruapepe:info@tamcare.or.tz**

DESEMBA 27, 2020
Nipashe
Baba, Mama na Mwana

# MAISHA Jumapili



Ukurasa 10

**Mtoto lazima ajifunze maneno machafu**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Pazia nalo linanogesha kama pambo la nyumba



## HARUSI

Ukurasa 12



## NGOZI INAYONG'ARA

# Kitunguu maji kinatosha kukupa furaha

Ukurasa 14

# Mtoto lazima ajifunze maneno machafu

Na Moses Ismail

MANENO machafu, au kwa lugha nyepesi tuliyozoea mitaani 'matusi', ni sehemu ya lugha ambayo lazima mtoto yeyote yule atajifunza tu, ili mradi anajumuika kucheza na watoto wenzake mtaani au shuleni.

Ataambiwa au atatukanwa na wenzake, atawasikia wenzake nao wakiwatusi wengine kwa maneno hayo ambayo wakati mwingine huwa makali zaidi. Yatamwingia akilini.



Kwa sababu hajui maana ya maneno hayo na kwa kuwa huenda yakawa yamemuuma au yanatembea kila wakati akilini mwake, hujikuta akilazimika kuja kukuuliza mzazi wake au mtu mzima mwingine, nini maana ya maneno hayo.

Kwa kuzingatia kuwa hajui kabisa maana ya maneno hayo na ni mtoto mwaminifu kabisa kwa wazazi wake, anapotaka kuuliza maana ya maneno hayo na anapoamua kukuuliza wewe mzazi wake, basi huwa haangalii upo na nani, atakuuliza tu.

Imeshawahi kutokea, pengine hata wewe unakumbukumbu zako, watoto wa aina hii wameshauliza maana ya maneno mazito kabisa kwa wazazi wao wakiwa mbele ya watu wazima wengine.

Katika hali kama hiyo na kwa kuzingatia uzito wa neno lenyewe, tusi, mzazi hujikuta akikereka na kumfokea mtoto huyo au wakati mwingine kumwadhibu kwa kumchapa bila ya kumweleza maana ya neno hilo.

Lakini unapotafakari kwa kina juu ya neno alilouliza, ingawa kweli ni tusi, hakupaswa kuchapwa hata kidogo. Hakupaswa kuchapwa kwa sababu kule kuthubutu kwake kuuliza maana ya neno hilo tu kunathibitisha kuwa hafahamu wala hajuu maana yake. Angejua asingethubutu kuuliza.

Katika hali kama hii, mtoto huyu anapaswa kusaidiwa kufahamishwa kwamba neno alilozungumza ni baya. Ni neno lisilotakiwa kuzungumzwa na mtu mwenye adabu, ni 'dhambi' kabisa!

Unawezaje kumweleza mtoto wako kwamba neno hilo aliloulizia kuwa ni neno baya asilopaswa kulizungumza ilhali tayari ameshakutia aibu mbele za watu? Unaweza kweli kuzuia 'kero' hiyo bila ya kumfokea? Ndio, inawezekana.

Inawezekana kwa kuanza kumuuliza kwa upole mno kama vile neno alilozungumza ni neno la kawaida tu lisilo na ubaya. Muulize; "nani amesema hivyo?" Atakapokueleza kuwa ni fulani, basi mweleze pia kwa upole tu kuwa neno hilo ni baya na ni dhambi kulisema tena.

Inawezekana mwanao asikuulize juu ya neno hilo, badala yake ukamsikia 'akimvugumishia' mwenzie neno la aina hiyo wakati wanacheza ama nje ya nyumba yenu au sebuleni. Naye pia usimfokee, muite na muulize na kisha umweleze kuwa neno hilo ni baya na ni dhambi kulitamka.

Katika hali ya kawaida ya maisha ya mwanadamu, maneno makali ni sehemu ya lugha inayomzunguka binadamu na lugha hii huwa tunajifunza tangu tukiwa wadogo na ndio maana sisi kama wazazi tunajua maneno mengi ya matusi kama sio yote.

Ni kwa njia zile zile tulizojifunza sisi, juu ya maneno hayo, ndio njia hizo hizo wanazopitia watoto wetu kujifunza lugha hizo. Ni lazima watoto wajifunze maneno makali. Ni sehemu ya maisha ya mwanadamu katika dunia yote.

## NA HAMIS KIDAGO 0657 207168 QUIZ

**Le Verbe Suivre – Kitenzi "Fuata"**

1. Kamilisha unyumbuaji wa kitenzi "Fuata" katika nyakati mbalimbali kama zilivyoainishwa hapo chini.

**Indicatif**

**present**
je suis
tu suis
il/elle suit
nous suivons
vous suivez
ils/elles suivent

**imparfait**
je suivais
tu suivais
il/elle suivait
nous suivions
vous suiviez
ils/elles suivaient

**futur simple**
je suivrai
tu suivras
il/elle suivra
nous suivrons
vous suivrez
ils/elles suivront

**passé simple**
je suivis
tu suivis
il/elle suivit
nous suivimes
vous suivites
ils/elles suivirent

**passé compose**
j' ai suivi
tu as suivi
il/elle a suivi
nous avons suivi
vous avez suivi
ils/elles ont suivi

**plus – que – parfait**
j' avais suivi
tu avais suivi
il/elle avait suivi
nous avions suivi
vous aviez suivi
ils/elles avaient suivi

**futur anterieur**
j' aurai suivi
tu auras suivi
il/elle aura suivi
nous aurons suivi
vous aurez suivi
ils/elles auront suivi

**passé anterieur**
j' eus suivi
tu eus suivi
il/elle eut suivi
nous eumes suivi
vous eutes suivi
ils/elles eurent suivi

**Conditionnel**

**present**
je suivrais
tu suivrais
il/elle suivrait
nous suivrions
vous suivriez
ils/elles suivraient

**passé**
j' aurais suivi
tu aurais suivi
il/elle aurait suivi
nous aurions suivi
vous auriez suivi
ils/elles auraient suivi

**Infinitif**

**present**
suivre

**passé**
avoir suivi


**Participe**

present
suivant

**passé**
suivi/ie
suivis/ies
ayant suivi

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

Jamaa mmoja alimtumia ujumbe mdogo wake kwamba anataka kwenda jijini Dar es Salaam, alimwomba amtajie sifa za maeneo yote.

**Jamaa:** Naomba nitajie sisa za Dar, kukoje maana nataka kuja?

**Rafiki:** Njoo tu huku hakuna shida, lakini maisha ya Dar tumeyazoea sisi wenyewe, nakushauri kaa huko huko kijijini ambako mnachinja kuku na kuliwa ndani ya nyumba hiyohiyo na utumbo mnatupa.

Huku Dar ni tofauti, kuku anachinjwa Kinondoni, shingo inaliwa Tandale, kidari Masaki, paja linaliwa Mikocheni, firigisi Magomeni, miguu inapendwa kutafunwa Mbagala, kipapatio uwaambii kitu Tandika, kichwa Manzese na utumbo Buguruni. Acha... chezea maisha ya Dar.

SWALI
Nazi inapatikana mikoa gani nchini Tanzania?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Roho ya ulevi inavyotesa wanandoa!

KARIBu tena msomaji wangu tuendelee kuzungusha hili gurudumu la Maisha Ndivyo Yalivyo. Bila shaka unafuatilia vema mada za safu hii kwa makini. Nimepokea ujumbe mbalimbali toka kwa wasomaji jinsi wanavyoelimika kwa yanayozungumzwa humu.

Leo tuzungumzie ulevi unavyotesa familia zetu hasa eneo la ndoa. Hii ni roho kubwa inayowaangamiza wanadamu wengi. Kuna uchawi wa ulevi wa pombe, bangi, sigara na kadhalika ambao unaweza kutupwa juu ya mtu na kumfanya asiwe na akili timamu.

Chanzo kingine cha ulevi ni pale mtu anawekewa uchawi kwenye pombe na kumfanya ashindwe kuacha kunywa pombe. Kuna roho za ulevi za kurithi hasa ulevi wa pombe. Hizi roho za kurithi hutokana na maagano yaliyowekwa na mababu kwenye koo zetu.

Madhara ya ulevi ni makubwa sana. Watu wengi wameangamia kwa ulevi, wengine wamepoteza maisha. Ndoa katika familia nyingi zimesambaratika kwa sababu ya roho ya ulevi. Hakika, ni roho inayopaswa kushughulikiwa kwa nguvu zote bila kuogopa ili mtu awekwe huru.

Msomaji wangu, baada ya utangulizi huo, hebu sasa nitoe mifano michache ya ndoa zilizoteswa na roho hiyo ya ulevi. Mizozo ya wanandoa walioathiriwa na ulevi imekuwa ikijitokeza hadharani na wakati mwingine ikifanyika kimya kimya kwenye maskani yao. Ukiona mizozo hii ikijitokeza wazi, ujue mtikisiko ni mkubwa.

Mama mmoja alishindwa kuvumilia tabia ya mume wake ya ulevi. Yeye ameokoka, lakini mumewe haamini katika habari ya kuokoka. Mama huyu akamwendea baba yake wa kiroho wa dhehebu analosali huku akilia machozi.

Akasema: "Mtumishi wa Mungu, mume wangu amenichosha kwa ulevi, nataka niachane naye kabisa mbele yako." Kiongozi huyu wa kiroho baada ya kumsikiliza ikabidi na mume huyo aitwe ili naye asikilizwe.

Walipokutanishwa huku wazazi wa pande zote wakiwamo, mke huyo wa ndoa akaanza kujieleza huku analia, akasema kwamba kwa tabia ya ulevi ya mumewe hawezi kuendelea kukaa kwenye ndoa.

Mume akaulizwa; Je, ni kweli una tabia ya ulevi? Akajibu, huwa nakunywa kwa kiasi tu. Mke akadakiza; "Muongo huyu ni mlevi hadi anarudi asubuhi...mimi namuacha leo hii." Mume naye akasema, "mimi simuachi, huyu ni mke wangu Mungu kanipa". Baada ya majibizano, baba yule wa kiroho ikabidi atumie hekima akamuuliza yule mume; Kama unataka mke huyu abaki kuwa mke wako, je, utakuwa tayari kuacha pombe baada ya kumalizika kikao hiki? Akajibu haraka; niko tayari mtumishi, siko radhi aniache!

Mpenzi msomaji, baada ya kikao kile yule baba aliacha kabisa kunywa pombe, na sasa hata afya yake imekuwa nzuri kwani alidhoofu kwa ulevi. Alikuwa hana muda wa kula ni yeye na pombe tu.

Kumbe inawezekana. Mama alipokomaa, jamaa akaona isiwe shida. Kuliko nimpoteza mama watoto bora nipoteze ulabu (unywaji). Sasa amani, furaha na utulivu vimerejea katika familia hiyo.

Mama mwingine akafikishana na mumewe kwa Ofisa Mtendaji. Mume akaanza; "Sitaki mke wangu akae na watoto kwani ni mlevi. Mama naye akadakiza; "Siyo kweli, anasema uongo. Yeye ndiye mlevi wa kupindukia. Upo wakati anarudi majogoo (alfajiri) na arudipo analala hadi na viatu na godoro linatota. Sasa nani mlevi hapo?"

Mpenzi msomaji, angalia jinsi ulevi unavyogonganisha vichwa wanandoa. Na ukweli ni kwamba wanaopata shida ni watoto wasio na hatia. Jambo ambalo wazazi wengi hawaelewi ni kwamba mizozo yao ambayo hufanyika wakati mwingine mbele za watoto, ni doa kubwa sana kwa maisha yao.

Mizozo hiyo ni chanzo kikubwa sana cha tabia hiyo kudakwa na watoto wao. Utaona mtoto anampiga mwenzake shuleni, kumbe ubaunsa aliuona kwa wazazi wake. Tuzuie watoto wasione mizozo kati ya wazazi na hasa inayotokana na ulevi ili kuwajenga katika misingi ya malezi yaliyo bora. Maisha Ndivyo Yalivyo!

***Bila shika msomaji wangu umejifunza jambo hapo. Naishia hapa kwa leo tukutane tena wiki ijayo. Je, unataka ushauri, maoni au una kisa cha kimaisha? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581. Pia namba hii ipo WhatsAPP.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Kufanya mchezo barabarani ni kuchezea roho za wengine

KIPINDI cha mwisho wa mwaka kunakuwa na idadi kubwa ya wasafiri ambao wanakwenda vijijini kwa ajili ya kukutana na familia zao katika sikukuu za mwisho wa mwaka.

Kutokana na adha ya usafiri wa umma, wengi wamejikuta wakipenda kutumia magari yao binafsi, ili kuepusha usumbufu na pia kusafiri kwa pamoja kama familia na kufurahi pamoja.

Barabarani wako madereva wa aina tofauti tofauti kama walivyo binadamu tofauti tofauti ambao licha ya kusoma sheria, taratibu na kanunu za matumizi ya vyombo vya moto barabarani, pamoja na vyuo sawa vya udereva, wako ambao ni tofauti na hufanya mambo tofauti kabisa.

Mathalani, juzi ilisambaa video ya abiria wa basi wakimshushia kipigo dereva wa lori ambaye aliwachomekea basi kiasi kwamba kama si dereva wa basi kulikwepa gari hilo, ingekuwa ajali mbaya sana.

Katika video hiyo abiria walikuwa wakali sana, huku wakimpiga dereva ambaye alionekana kukimbia huku na kule lakini bado walimfuata na kumshushia kipigo kikali, huku wakieleza kuwa alitaka kuwaua kwa kuchomekea.

Tabia ya kuchomekea mara nyingi huwa makusudi ya madereva wa magari makubwa ambao hufanya hivyo kwa kuwa wanajua watasababisha ajali hiyo na kukimbia huku wakiacha majanga nyuma na wengi ni katika ujinga wa kutaka kuonyesha ubora wa chombo cha moto anachotumia au ubabe wake kuwa anaweza kuendesha kwa kasi.

Hii kufanywa na madereva ambao kichwani hapajakamilika vizuri na suala la utu bado halipo ndani yao kwamba unafurahi kuchomekea ili wengine waumie jambo ambalo halina manufaa yoyote kwa anayefanya hivyo bali majuto kwa kuwa katika gari hilo wamo ndugu, jamaa na marafiki ambao sote ni Watanzania.

Hakuna asiyejua madhara ya ajali yoyote ya gari ambayo hugharimu mhusika kisaikolojia, kwa kipato cha famili kitatumika umtibu na kama alikuwa ndiye anategemewa na familia basi familia yote imeporomoka. Huo unakuwa ndio mwanzo wa watoto kutokwenda shuleni, kukosa mahitaji ya msingi ya familia, hatalipa kodi na kama alikuwa na miradi basi itasimama.

Wako ambao wanasota hospitalini kwa miaka mingi na wameshauza mali zote za familia, wamefukuzwa kazi na sasa hawana kipato chochote cha kutunza familia, chanzo kikiwa ni ajali ambazo mtu aliamua kufanya uzembe kama wa huyo dereva.

Mathalani, siku moja wakati nasafiri nilisimamishwa na trafiki akiniomba kumbeba abiria mmoja ambaye alikuwa amchafuka sana. Baada ya kumbeba niliuliza kulikoni akanieleza kuwa aliondoka Dar es Salaam alfajiri sana akienda Moshi na ghafla alichomekewa na lori kiasi cha gari yao kupinduka mara tatu.

Walikuwa watu wanne ndani ya gari na kwa kudra za Mwenyezi Mungu, wote walipona ila gari liliharibika kabisa, jambo ambalo ni hasara kubwa kwao na iliwapotezea muda na mpango wa kuendelea na safari yao.

Ukiangalia jambo hili linafanana na dereva wa lori aliyelichomekea basi lakini kwa kuwa kulikuwa na nafasi ya kukwepa dereva wa basi alifanikiwa kufanya hivyo, lakini kwa mwenye gari dogo hakukuwa na nafasi na kujikuta anapinduka.

Hili ni jambo baya sana kwa kuwa uamuzi wa kijinga ya sekunde moja unagharimu maisha ya mamia ya watu. Kutokana na hali hiyo, wazazi wanaumia, wanafariki dunia, taifa linapata hasara ya miundombinu na nguvu kazi ambayo ni walipakodi.

> **"Walikuwa watu wanne ndani ya gari na kwa kudra za Mwenyezi Mungu, wote walipona ila gari liliharibika kabisa, jambo ambalo ni hasara kubwa kwao na iliwapotezea muda na mpango wa kuendelea na safari yao.**

Ni vyema madereva wakafikiri mara nyingi sana kabla ya kufanya uamuzi wowote, ni muhimu kuwa na udereva wa kijihami, udereva unaojali watumiaji wengine wa barabara, kuwafikiria wengine na kujiona kama ni mimi ningefanyiwa hivyo ingekuwaje kuliko kufanya kwa sifa au ubabe.

Wakati mingine kuna tabia ya baadhi ya madereva kufanya mashindano barabarani kwamba kwa nini gari fulani la aina fulani limenipita barabarani, naye anafanya kila awezavyo kulipita au wakati mwingine malori au mabasi kuona kwa nini gari dogo limpite au gari dogo kushindana mwendo na basi au lori, jambo ambalo si sawa kabisa.

Baadhi ya madereva wamesababisha vifo, majeruhi kwa sababu ya matendo kama hayo ambayo moja kwa moja mtu akikaa na kutafakari atajilaumu maisha yake yote, ni muhimu sana kuwa makini na kujali watumiaji wote wa barabara.

Kwa kipindi hiki ni muhimu sana kuwa na tahadhari, kufuata sheria za uendeshaji wa chombo cha moto, udereva wa kujihami na unaojali watumiaji wengine wa barabara ili kuendelea kuwa salama.

***Tutafakari!***

***Mungu Ibariki Afrika***
***Mungu Ibariki Tanzania***

# HARUSI



**Agusta Njoji na Alex Sonna**

Ndoa ilifungwa Kanisa la Mt. Gemma Galgan Nkuhungu, Dodoma, Desemba 12, 2020.



# MITINDO






## KOFIA GANI Inakutoa bomba?

KWA watu wanaothamini mwonekano wao, kila wakati wanabuni njia za kuwafanya kuwa tofauti kwa kuwa na vionjo vinanayokwenda na wakati.

Moja ya kionjo ambacho kinapendwa na wengi katika kunogesha mwonekano wao ni kofia. Vazi hili la ziada linavaliwa na watu wa jinsi zote na mara nyingi hutumia aina mbalimbali za kofia.

Kwa ujumla uvaaji wa kofia unambadilisha mtu husika taswira yake kwa haraka pamoja na kumjenga mwonekano unaovutia.

Wataalamu wa masuala ya urembo wanasema uvaaji wa kofia pamoja na kupendezesha sura, pia inalinda nywele kuathirika na miale ya jua.

**JINSI YA KUTUMIA**

Kwa kawaida kufia aina ya kapelo haichagui haina ya nguo, lakini ni vizuri ikatumika na nguo zinazoendana nazo pamoja na wakati.

Kofia ya aina hii hairuhusiwi kuvaa sehemu za kazi au ofisi za kiserikali na kama zikitumika inakuwa katika shughuli maalum za kitaifa, kisiasa, kitamaduni na kijamii.


Hata hivyo kundi la vijana hasa wasanii wamekuwa wakivaa na kuzidisha mvuto wa vazi hilo kwa watu wengine.

**UNAPONUNUA**

Wakati unapofikiria kununua kofia ya kapelo, hakikisha unakuwa makini kwa kuangalia ubora wake na rangi unayopenda.

Hakikisha ukubwa wa kofia unalingana na kichwa chako, usinunue kubwa kwani haitakuletea matokeo mazuri. Pia kofia isikubane sana na kukuletea usumbufu pale unapovaa.

UREMBO



NGOZI INAYONG'ARA

# Kitunguu maji kinatosha kukupa furaha

KITUNGUU ni miongoni mwa viungo ambavyo hutumika kuongeza ladha katika vyakula vya aina mbalimbali pamoja na mafuta yake kuwa tiba nzuri kwa binadamu.

Kwa wale wanaopenda kula jibini, kitunguu ni moja ya sehemu ya mboga ya majani inayoleta harufu na ladha nzuri wakati wa kula.

Hata hivyo, wataalamu wanasema kuna matumizi zaidi hayo, kwani kitunguu kina mchango mkubwa katika ulimwengu wa ulimbwende.

Kwa mujibu wa wataalamu hao, kitunguu kikiliwa kila siku haichukui muda mrefu kuona matokeo mazuri katika afya ya ngozi kwa kuondoa magonjwa kutokana na virutubisho vilivyomo ndani yake.

Kwa matumizi ya kitunguu pekee, husababisha ngozi ya mtu kuwa na nuru na mng'aro unaovutia.

Ili kujua nguvu ya kitunguu katika urembo unatakiwa ufuate hatua zifuatazo.

**HATUA ZA KUFUATA**

Chukua kitunguu na ukikate katikati na kisha kukiminya ili kutoa majimaji ambayo utatumia kujipaka mwilini.

Unaweza kuwa kama utaratibu wako wa kujipaka mara moja angalau kwa wiki moja ili kupata matokeo ya haraka. Hakikisha unapopaka unakaa kwa dakika kadhaa, na baada ya hapo unaweza kwenda kuoga kwa kutumia majisafi na sabuni ambayo itaondoa harufu ya kitunguu.

Kama ukitumia kulingana na mahitaji yako, haraka utaona ngozi inabadilika na kuwa laini na yenye mng'aro wa kupendeza. Hakikisha unaacha ngozi yako katika uasilia ili kujiweka katika Uafrika zaidi.

MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

PILAU YA NYAMA

# Furahia X-Mas na Mwaka Mpya



MSIMU wa sikuu za Krismasi na Mwaka Mpya umewadia hivyo familia nyingi zinajumuika nyumbani.

Wapo waliosafiri kurudi makwao kujumuika na ndugu na jamaa kwa ajili ya kula sikukuu, na waliopo mijini wao hukaa na familia zao au hutembeleana ndugu jamaa wakiwa na furaha tele.

Katika wiki hizi mbili za mfululizo wa sikuu, mambo yanakuwa hayaendi watu hawasikii raha kama pilau na nyama havijapikwa.

Katika kipindi hiki familia nyingi zinapembelea kula vyakula mbalimbali lakini bila kukosa pilau na nyama iwe ya ng'ombe, mbuzi au kuku ili mradi tu iwepo.

Katika safu yetu leo tunakumbushana tu mambo ya kuzingatia wakati wa kupika pilau na kuandaa nyama. Mara nyingi pilau linanoga likiwekwa nyama na viazi na wengi wanaenda mbali na kunogesha na njegere kwa mbali.

Wakati wa kupika pilau lako hakikisha unakuwa makini usizidishe maji pilau likaharibika na kuwa bokoboko halinogi tena kiukweli.

Pia hakikisha unakadiria viungo vyako kulingana na kiasi cha mchele na nyama uliyoandaa, pilau ikiwa na maviungo mengi halipendezi hata kidogo kwanza linakinaisha.

Pia usisahau kuwa makini na chumvi na mafuta visizidi ikawa kero. Bila kusahau kuwa makini chakula chako kisiungue au usipunguze moto kikaiva upande watu wakala vibichi wakavimbilwa.

Kwa upande wa nyama wapo wanaopenda kukaanga, kuchoma na wengine kuoka na mvuke.

Katika kuhakikisha mnafurahia wanyama mnaotaka kuwafaidi sikukuu hizi, hakikisha unandaa nyama yako mapema na uweke viungo vya kutosha kabla ya kukaanga au kuchoma ili ziive taratibu.

Kumbuka ukichelewa kuandaa kitoweo chako mapema, utafanya haraka na muda wa kula utafika watu watakula nyama mbichi au ambayo haijakolea viungo.

Pia wakati huu wa sikukuu zingatia muda wa kuandaa vyakula vyote ili watu wale kwa wakati na kufurahia sikukuu vyema.

## MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Pazia nalo linanogesha kama pambo la nyumba

PAZIA ni miongoni mwa pambo linalotumika sana kupendezesha nyumba.

Kama ilivyozoeleka, pazia limekuwa likitumika kupambwa mlangoni na dirishani.

Hasa katika sehemu zenye joto kali ambazo mara nyingi madirisha yake huwa yenye wavu, pazia hutumika sana.

Lakini hata katika sehemu ambazo madirisha yake ni yale yasiyo na wavu, bado wanatumia pazia kama pambo la kupendezesha nyumba na miaka ya hivi karibuni limekuwa likitumika zaidi kuliko miaka ya nyuma.

Si tu nyumbani, bali katika sehemu za ofisi, hotelini na sehemu nyingine, pazia limekuwa likitumika kama kuziba, lakini kama pambo.

Siku hizi tofauti na miaka ya nyuma, baadhi ya familia hupendelea hata wakati mwingine ndani ya nyumba kunapokuwa na mapazia mazuri yenye mvuto, hulazimika kugharimia kuweka kiyoyozi ili pazia isivurugike katika mpangilio wake na kuharibu mvuto wa ndani ya nyumba.

Zipo pazia zilizotengenezwa kwa kutumia kitambaa kizito sana, za kati na nyepesi zaidi.

Lakini kuna mapazia ambayo yanamatobo, lakini yote yanatumika kupamba nyumba, ofisi ama hoteli kulingana na mahitaji ama mandhari katika sehemu husika.

Katika kutumia pambo hilo la pazia kwenye nyumba, hakikisha unachagua ambalo rangi zake inaendana na zile zilizopo katika nyumba yako.

Si lazima lifanane na rangi zote za ndani ya nyumba, lakini hata kama ni mojawapo ya zile zilizopo ndani itapendeza tu.

Zingatia pia rangi ambazo hazing`ai sana ambazo hazileti utulivu ndani ya nyumba.

## MPANGILIO


### Dondoo muhimu katika kuchagua marumaru sahihi

**1:** Tazama bajeti yako kama inaweza kukidhi ukubwa wa nyumba au chumba chako.


**2:** Angalia bei ya marumaru kama inalingana na bajeti yako, kama ni kubwa angalia namna ya kuifikia au kusitisha.

**3:** Rangi ni jambo muhimu la kuiangalia, hakikisha unachagua rangi nzuri ambayo itang'arisha nyumba vizuri.

**4:** Ubora wa marumaru ni suala lingine la kuwa nalo makini, hakikisha ubora wa bidhaa unakuwa wa hali ya juu kulingana na bei husika.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2020
SMS - 0621 412 879
UNAFUKUZA MUAMALA!!! MWENZAKO NIME-AGA KWA WAIFU NIPO KWETU MKOA KUHESABIWA
MIMI NI KAHABA MWENYE HURUMA NILICHOKUKAMUA TOKA KRISSMASI KINATOSHA
BUZA
ONDOKA BABA NITOKE NIENDE KUHANGAIKA
HANGAIKA HUMOUMO UNIPE KODI YANGU NIKAFUNGE BAR
UZURI WA JEMBE UAMUE MWENYEWE LAKINI ISIWE KWA AJILI YA KUTAFUTA NAULI KURUDI MJINI
MKOA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
JUKWAANI
KUMBE JOTO KALI HALITOKANI NA HALI YA HEWA PEKEE! UKAPUKU NAO UNACHANGIA
BAR NAZIPITIA MBALI KAMA 'PEMBE ZA NDOVU!!'
WEEE! NILIPOKUJA KUKOPA SIJAKUNJA NGUMI, NILITUMIA MANENO LAINI...
USINIFUNDISHE KUDAI DENI LA KUSUKUTUA BIA MWAKA MPYA
DEREVA POLEPOLE MWISHO WA MWAKA USITAKE TUSIVUKE WENZAKO
KWA HIYO ZIRAILI YUPO MWISHO WA MWAKA TU?!
...SHANGILIA MWAKA USITUKERE WENZAKO...

HABARI KIMATAIFA

## Watu waliouawa Ethiopia wafikia 207

**ADIS ABABA,** ETHIOPIA

TUME ya Kutetea Haki za Binadamu nchini Ethiopia (EHRC) imesema watu 207 waliuawa katika shambulio lililofanywa na watu wenye silaha magharibi mwa nchi hiyo.

Idadi hiyo mpya ni zaidi ya mara mbili ya iliyotolewa awali na serikali.

Tume hiyo ilisema mnamo Jumatano ya wiki hii, watu 100 waliuawa wakiwa wamelala ndani ya nyumba zao na mashamba yao kuchomwa moto katika shambulio lilotekelezwa majira ya alfajiri katika eneo la Metekel, katika mkoa wa Benishangul-Gumuz.

Kupitia mtandao wao wa Twitter, EHRC iliandika kuwa watu hao, 133 walikuwa ni wanaume, wanawake 35 na watoto 17.

Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, kupitia mtandao wake wa Twitter, alisema amesikitishwa na mauaji hayo na kukiri kwamba juhudi za serikali za kutatua tatizo hilo zimeshindwa kufaulu.

**DW**

## China yajipongeza mapambano Covid-19

**BEIJING,** CHINA

VIONGOZI wa chama tawala cha kikomunisti nchini China, wamejipongeza kwa mafanikio waliyoyapata katika kushughulikia mlipuko wa virusi vya corona.

Chombo cha juu chenye kufanya maamuzi ya chama, kilisema uongozi wa chama hicho ulitekeleza jukumu muhimu la kupambana na virusi vya corona mwaka huu.

Nchi iliyopo Mashariki mwa Asia, ilifanikiwa kwa kiwango kikubwa kudhibiti kusambaa kwa ugonjwa wa Covid-19 na imekuwa moja ya nchi iliyoripoti ukuaji wa uchumi mwaka huu licha ya nchi nyingine duniani kuathirika kiuchumi.

Hata hivyo, ilishtumiwa vikali kwa kutotoa taarifa sahihi juu ya mlipuko wa virusi vya corona, virusi navyoaminika kuanzia katika mji wa kibiashara wa Wuhan mnamo mwezi Desemba mwaka uliopita.

**DW**

# Watu zaidi ya 11 wameuawa Nigeria

**ABUJA,** NIGERIA

VYANZO vya habari katika eneo hilo vinasema wapiganaji waliingia katika kijiji cha Pemi Jimbo la Borno usiku wa mkesha wa Krismasi, kwa kutumia magari na piki piki na kuanza kufyatua risasi kiholela.

Pemi iko karibu na Chibok ambako wasichana 200 wa shule walitekwa mwaka 2014.

Boko Haram wamefanya mashambulio kadhaa kaskazini mwa nchi hiyo, ambao wanalenga kupindua serikali ili kubuni taifa lao la Kiislamu.

Shambulio hilo lilotokea Alhamisi, lilitabiriwa na maofisa wa usalama ambao walisema huenda kukatokea mashambulio hasa wakati wa sikukuu ya Wakristo.

Baadhi ya wanavijiji walitorokea msituni na idadi kubwa bado hawajulikani waliko.

"Magaidi waliwaua watu saba, kuchoma moto nyumba 10 na kuiba bidhaa za chakula ambazo zilikuwa zigawanywe wakazi wakati wa sherehe ya Krismasi," kiongozi wa wanamgambo Abwaku Kabu alisema.

Washambuliaji hao walichoma moto kanisa, kumteka mchungaji na kuiba bidhaa za matibabu katika hospitali moja kabla ya kuiteketeza moto.

Hivi karibuni, kundi hilo lilidai kuwateka nyara wavulana zaidi ya 300 wa katika Jimbo la Katsina.

Vurugu za Boko Haram ambazo zimedumu kwa miongo kadhaa, zimesababisha kuuawa kwa watu karibu 36,000 na wengine milioni mbili kukimbia makazi yao, kulingana na Umoja wa Mataifa.

Katika kujilinda, jamii katika eneo hilo zimeamua kubuni vikundi vya kujihami na wanamgambo ambao wanafanya kazi kwa ushirikianao na wanajeshi wa serikali.

Hivi karibuni, kundi hilo lilidai kuwateka nyara wavulana zaidi ya 300 katika Jimbo la Katsina, hata hivyo serikali ya nchi hiyo ilisema waliohusika na utekaji huo ni magenge ya wahalifu wanaoshirikiana na wanamgambo wa Kislam.

**BBC**



Baadhi ya wakazi wa Accra nchini Ghana wakiwa katika ufukwe wa bahari eneo la Sakumono, wakifurahia sikukuu ya Krismasi. Nchi hiyo imekuwa katika masharti magumu ya kutojumuika watu wengi kujikinga na Covid-19.

# Wanajeshi wa Burundi wauawa Afrika ya Kati

**BANGUI,** AFRIKA YA KATI

WANAJESHI watatu wa Umoja wa Mataifa wanaolinda amani Jamhuri ya Afrika ya Kati, wameuawa na waasi, wakati nchi hiyo leo inafanya uchaguzi wake mkuu.

Taarifa iliyotolewa na umoja huo, ilisema kuwa wanajeshi hao waliofariki dunia wanatokea Burundi na wenzao wawili wamejeruhiwa kufuatia uvamizi uliofanywa na waasia hao katika kambi ya vikosi vya Umoja wa Mataifa na serikali.

Ilieleza kuwa uvamizi huo ulifanyika kwenye mji wa Dekoa mkoani Kemo na mji wa Bakouma kusini mwa mkoa wa Mbomou.

Msemaji wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Stephane, alilaani vikali mashambulizi hayo na kuzitaka mamlaka nchini Jamhuri ya Afrika ya Kati kuchunguza kile alichokiita uvamizi wa kikatili.

Pia alionya kwamba mashambulizi dhidi ya walinda amani yanaweza kuchukuliwa ni uhalifu wa kivita.

Taarifa hizo zimekuja katika wakati ambapo muungano wa waasi umetangaza kusitisha mapigano na kusema utaendelea na maandamano yake kwenye mji mkuu wa Bangui.

Vikosi vya wanajeshi kutoka Rwanda na Urusi vimewasili nchini humo kwa ajili ya kuongeza nguvu kuisaidia serikali ya taifa hilo kuondolewa madarakani kwa nguvu.

Rais Faustin Archange Touadera, ambaye anawania tena wadhifa huo, amemtuhumu mtangulizi wake, Francois Bozize, kwa kupanga njama ya mapinduzi.

Hata hivyo, Bozize, ambaye amewekewa vikwazo na Umoja wa Mataifa na pia alizuwia na Mahakama ya Katiba kuwania urais, anakanusha shutuma hizo.

Jumanne, kundi moja la wanamgambo liliuteka kwa muda mji wa nne kwa ukubwa nchini humo kabla ya kukombolewa na askari wa walinda amani.

**DW**

## MAKALA

# Tuyatafakari haya



Na Magabilo Masambu

**Zamani mtu kama hajui mahali alikuwa anauliza na anapelekwa, lakini siku hizi hata kumuuliza mtu kwa fulani ni wapi unaogopa maana ukigundulika kwamba wewe ni mgeni katika eneo hilo unaweza kufanywa chochote.**

MAKALA hii ikiwa ni ya mwisho kwa mwaka 2020, tuna kila sababu ya kuyatafakari baadhi ya mambo ili kwa neema ya Mungu, tunapouanza mwaka mpya wa 2021, tuwe na dira ya mambo gani ya kurekebisha kwa ajili ya ustawi wa taifa letu la Tanzania.

Jambo la kwanza ni umoja wetu. Kumekuwapo na kila aina za dalili zinazoonyesha kwamba kwa kipindi sasa mpaka mwaka huu, umoja wetu kama Watanzania umeanza kuyumba kama ni nyakati zile za Mwalimu Julius Nyerere tungeita ufa na kama hatutauziba, unaweza kubomoa nyumba.

Nyufa katika nyumba huwa zinaweza kuonekana katika msingi, ukuta au hata kwenye paa. Nyufa za umoja wetu kuyumba, zimeanza kuonekana katika siasa na zinakwenda mbali zaidi hata katika shughuli za kijamii.

Siku hizi limekuwa jambo la kawaida sana kuona watu wanahudhuria mazishi kwa misingi ya itikadi za kisiasa jambo ambalo hatukuwa nalo huko nyuma. Mbaya zaidi na sare za vyama zinavaliwa wala hakuna anayeshtuka. Pengine linaweza kuonekana jambo la kawaida lakini lina maana gani hasa katika maisha yetu ya kila siku? Zamani tulizikana bila kujali unatoka chama gani. Tukimaliza siasa kundi gani litafuata?

Pili ni utu. Miaka ya hivi karibuni imekuwa kawaida kusikia kwenye vyombo vya habari kuhusu matukio ya kutisha katika maeneo mbalimbali ya nchi yahusuyo binadamu kama vile kuuana, kudhulumiana, ubakaji, unyanyasaji wa kijinsia na mengine kama hayo. Mambo haya kutokea ni dalili za watu kujaa roho za kinyama na kupoteza tena thamani ya utu!

Tofauti ya binadamu na wanyama ni utashi. Mtu akikosa utashi, atakuwa sawa kabisa na mbuzi. Naona dalili za binadamu kuishi kama wanyama badala ya watu. Zamani mtu kama hajui mahali alikuwa anauliza na anapelekwa, lakini siku hizi hata kumuuliza mtu kwa fulani ni wapi unaogopa maana ukigundulika kwamba wewe ni mgeni katika eneo hilo unaweza kufanywa chochote. Tunakwama wapi? Tatizo ni nini? Mbona hatukuwa hivi?

Jambo la tatu ni ukarimu. Kumekuwa na mijadala mingi juu ya ukarimu wetu katika jamii. Wengine wanasema watu wamekuwa na roho za ubinafsi sana kuliko zamani, huku wengine wakisema maisha yamekuwa magumu tofauti na zamani pesa mbele utu nyuma.

Nakumbuka zamani zile, wazazi walikuwa wakivuna mazao yao walitupatia kiasi fulani kuwapelekea walimu kama shukrani na walimu waliheshimika sana hasa maeneo ya vijijini kutokana na kazi yao ya kuandaa maisha ya wengine. Leo walimu na wazazi wanaishi kama paka na panya.

Pia wakati tunaumaliza mwaka, tutafakari malezi yetu pengine ndicho chanzo cha yote haya. Malezi na maadili ni vitu viwili vinayotegemeana. Malezi mabovu hutengeneza maadili mabovu na maadili mabovu hutengeneza malezi mabaya. Mleaji anapaswa kuwa na maadili mazuri. Iwapo baba, mama na jamii kwa ujumla tutakosa maadili mazuri, kwa vyovyote vile malezi lazima yatakuwa mabovu.

Siku hizi, wazee tunawalaumu vijana kwa kuwa na tabia za ovyo. Lakini tunasahau kwamba malezi hayo yanatokana na maadili yetu mabaya. Ni jambo la kawaida siku hizi mzee kusalimiwa shikamoo na kijana, halafu anaitikia mambo vipi! Halafu kesho kijana akimwambia mzee mambo vipi, utasikia mzee akisema huyu kijana hana adabu.

Wako wanaosema salamu ya shikamoo ni ya kikoloni, hivyo haina maana na sasa hata kwenye familia zao, wanasalimiana mambo vipi mshikaji na kwamba "Uzee mwisho Msoga" Mkubwa na mdogo hajulikani tena, wanajiita watoto wa kishua. Hapa Arusha utasikia wanaitana dingilai! Hii ni hatari sana.

Ni ukweli kwamba dunia na maisha vimebadilika. Lakini kama Watanzania tunao uwezo wa kuchagua lipi linatufaa kulingana na mila, desturi na utamaduni wetu, hatuwezi kuzoa kila kitu kikawa chema kwetu. Nakiri kwamba si kila mila za kitanzania ni nzuri. Mbaya tunaachana nazo, nzuri tunaendelea nazo bila kuathiriwa na mabadiliko ya kidunia.

Mfano mdogo tu, tunao utamaduni wa kula chakula pamoja kwenye familia. Kama ni ugali unawekwa kwenye sahani moja na wakati unamega tonge, tulifundishwa ni marufuku kuvusha mkono ukamege upande wa mwenzio. Siku hizi anayewahi ndiye anakula kikubwa, tutazuia ufisadi serikalini kweli?

Zamani ulikuwa ukipiga yowe, watu walikuwa wakitoka kuja kufahamu nini kimekupata, siku hizi ikisikika yowe kila mmoja anajifungia vizuri. Tumepoteza umoja na upendo wetu. Mwaka 2021 uwe mwaka wa mabadiliko. Yako mengi sana lakini tuyatafakari haya.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Unakumbuka enzi za kuruka ukuta Uwanja wa Taifa?



Na Adam Fungamwango

**Hii ikanikumbusha miaka mingi nyuma. Miaka ya 1980 katika Jiji la Dar es Salaam na mikoa mingine, watoto wengi waliokuwa na kiu ya kupenda soka, lakini hawana uwezo wa kuingia. Walibuni mbinu kali ya kuruka ukuta na kuingia ndani licha ya ulinzi mkali wa polisi, waliokuwa na farasi na mbwa wakati huo.**

UKIWA unatazama mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, wakati mwingine kamera huwa zinahamishwa uwanjani na kupelekwa kwenye matukio mbalimbali ndani na nje ya uwanja.

Moja ya mambo ambayo yanawavutia watamaji wengi, mbali na kuwa ni jambo la hatari sana ni pale wanapoonekana baadhi ya mashabiki wako juu ya miti, lakini wanaangalia mpira.

Miti hiyo inakuwa iko nje ya uwanja lakini baadhi ya mashabiki ambao hawajajaliwa kuwa na pesa za viingilio wakati huo, wanakuwa wamepanda juu ya miti na kung'ang'ania huko kila mtu na staili yake, ili mradi tu aone mechi. Na mara nyingi huwa ni mechi zinazozihusu klabu kubwa mbili nchini zenye mashabiki wengi, Simba na Yanga.

Timu hizi zimejaliwa kuwa na mashabiki wengi kila kona ya nchi, hivyo popote zinapokwenda kucheza mikoani hujitokeza mashabiki wengi mno kutaka kuangalia mechi na kuona wachezaji, wakati mwingine kuliko hata Dar es Salaam.

Hiyo kwenye miti ni dibaji tu. Wako wanakuwa wamepanda kwenye maghorofa mbalimbali ambayo bado yanatengezwa. Nimeshawahi kuona baadhi ya mashabiki wameparamia nguzo zile kubwa za chuma za umeme, wako juu wakiangalia moja kati ya mechi za Ligi Kuu.

Nasema ni mambo ya hatari sana, lakini mashabiki wa soka wakati mwingine huwa kama 'vichaa' linapokuja jambo la mpira wa miguu, hasa timu wanazozipenda. Huwa hawajali.

Mikoa mingine utaona watu kwenye milima, wakiwa wamekaa juu wakifuatilia mechi kama kawaida, kuna mikoa yenye mawe makubwa kama Mwanza na Singida. Nako utaona watu wako juu ya mawe. Wametulia tuli wanaangalia kabumbu.

Hii ikanikumbusha miaka mingi nyuma. Miaka ya 1980 katika Jiji la Dar es Salaam na mikoa mingine, watoto wengi waliokuwa na kiu ya kupenda soka, lakini hawana uwezo wa kuingia. Walibuni mbinu kali ya kuruka ukuta na kuingia ndani licha ya ulinzi mkali wa polisi, waliokuwa na farasi na mbwa wakati huo.

Mfano wa leo ni ule wa watoto wadogo kuanzia miaka saba hadi 15 wakati huo walivyokuwa watundu ambao walikuwa na uwezo wa kutoka mbali na kwenda uwanjani bila ya kuwa na nauli na wala pesa za kuingia uwanjani.

Lakini huwezi kuamini, wanasafiri au wanatembea kwa miguu. Wakifika uwanjani wataingia na kukaa eneo la mbele kabisa karibuni na chaki za uwanja sehemu za kuchezea na mechi ikiisha watarudi nyumbani bila matatizo na mechi inayofuata watafanya vivyo hivyo.

Wale wa Dar es Salaam, mara nyingi baadhi walikuwa wakibania pesa wanazopewa za kutumia shuleni au hata zile wanazopewa na ndugu na jamaa. Hizo ni kwa ajili ya nauli tu.

Wakati mwigine kama hawana pesa kundi la watoto linaanza kuondoka kwa miguu kutoka sehemu wanazoishi na kwenda Uwanja wa Taifa ambao kwa sasa unajulikana kama Uwanja wa Uhuru.

Kumbuka kuwa kipindi hicho hata mabasi hayakuwa mengi kama sasa, hivyo kulikuwa na shida ya usafiri na watoto walikuwa wanatoka mbali mfano Kigogo, Mburahati, Ubungo, Tandale, Magomeni, Mbagala, Mtoni, Temeka, Tandika, Kongowe kwenda kuangalia mechi Uwanja wa Taifa.

Nilichogundua baadaye ni kwamba watoto wa wakati ule, hawakuwa wanachagua mechi, si mpaka icheze Simba na timu fulani au Yanga na timu nyingine. Hata timu zingine zikicheza Pilsner na Nyota Nyekundu, au Sigara na Pan African wao wapo tu.

Burudani ni pale wanapofika eneo la uwanja. Watoto hugawanyika vikundi. Wengine watapanda upande wa kushoto mwa ukuta na wengine upande wa kulia.

Wote hao lengo ni moja tu kuruka chini na kuelekea uwanjani. Watoto wa zamani walikuwa watundu sana. Kama unaufahamu ukuta wa Uwanja wa Taifa, ni mrefu sana. Hata kwa mtu mzima kuparamia na kuruka chini upande wa pili ni ngumu sana, achilia mbali mtoto. Halafu chini wanapotaka kurukia kuna maafande waliokuwa wanalinda. Wengine wana mbwa pia.

Mluzi utapigwa. Wa upande mmoja wataruka chini kwa pamoja na kuanza kukimbia kuelekea uwanjani. Wakati polisi wanakuwa wamehamasika na kutaka kuwakimbiza na upande wa pili nao wanakuwa wamepata nafasi na wao kuruka pia. Hii ilikuwa inawachanganya mno maafande, hivyo watoto wengi wanakuwa wanaingia uwanjani.

Staili hii ni kama nyumbu. Wako wachache kama wawili au watatu watakaokamatwa, lakini wengi watapita. Na watapata adhabu kidogo kama kupigwa fimbo au kulazwa chali au kifudifudi wakati mechi inaendelea, lakini baadaye wataachiwa.

Hii ilikuwa ndiyo staili ya maisha ya watoto wengi wapenda soka kipindi kile. Ilikuwa ndiyo tabia yao na maisha yao. Na mara kwa mara walikuwa wakibuni staili tofauti tofauti za kuwalaghai askari wakapoparamia ukuta ili kuingia uwanjani.

Tabia hii ilifika kikomo pale alipochaguliwa mwanamama Fatuma Said Ali kuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Utamaduni, Vijana na Michezo. Sijui alikuwa anaona au anaambiwa vituko hivyo kwa watoto.

Yeye akaamuru watoto wote kuanzia miaka 10 kurudi chini waingie bure mpirani. Na hii ni kwa ajili ya kuwafanya wapende zaidi soka wakiwa bado wadogo, waige yale wanayoyaona kwa wachezaji wakubwa uwanjani, ili taifa liwe na wachezaji wengi wazuri baadaye.

# HADITHI

MILIO mitatu ya risasi ilisikika maeneo ya Keko Bora jijini Dar es Salaam. Sauti hizo za risasi ziliwafanya watu kutimua mbio na kutafuta chaka la kujificha. Kila mmoja alidhani ni majambazi waliovamia kwa ajili ya kupora pesa dukani au kwenye vibanda vya mawakala wa kampuni za simu. Haikuwa hivyo. Yeyote aliyedhani ni majambazi alikosea. Aliteremka mtu mmoja kwenye gari na alichofanya ni kumpora mwanamke aliyekuwa kwenye kituo cha basi mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja tu na kuondoka naye. Huyu jamaa aliyefanya hivyo ni nani? Ni kwa nini amepora mtoto? Mtoto ni wa nani? Mwanamke aliyeporwa mtoto anamfahamu mporaji?

# Nina Jambo Langu-2

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

MIMI nilikuwa nimesimama hapa na mume wangu huyu, akaja mtu mmoja mrefu, akapiga risasi juu na kuninyang'anya mtoto, akaondoka naye." Alisema dada huyo ambaye sasa alikuwa amekaa chini kabisa baada ya kuonekana kukosa nguvu kutokana na woga, kulia na kufadhaika.

"Huwezi kuwa unamfahamu mtu huyo?" Mwingine aliuliza.

"Hapana simfahamu, halafu pia alikuwa amevaa mawani." Alijibu kwa kwikwi.

"Basi hapa cha kufanya kwanza kabisa ni lazima kwanza mkapige ripoti polisi mengine yafuate baadaye." Mwingine alidakia.

"Wewe ndiye mume wa huyu dada?" Bado watu walizidi kuuliza maswali.

"Ndiyo, tulikuwa tumetoka nyumbani, mtoto alikuwa anaumwa na hivi tulikuwa tunampeleka hospitalini, hapa tulikuwa tunasubiri daladala kwenye Hospitali ya Amana, lakini ndiyo tumekutana na haya yaliyotukuta." Alisema aliyeonekana kuwa ni mume wa dada aliyeporwa mtoto.

Hapo sasa kila mmoja alikuwa na tafsiri yake. "Inaonekana labda jamaa kaja kumpora mtoto wake, labda huyo mumewe kabambikiwa tu, jamaa anazinguliwa mtoto wake, sasa kaamua kuja kumchukua kwa nguvu."

Hizo zilikuwa ni dhana baada ya tukio hilo la aina yake kutokea. Katika sakata hilo ni mtu mmoja tu aliyeliona tukio hilo kwa usahihi zaidi.

Alimwona dada huyo na mumewe walivyokuwa wamevuka barabara na kwenda hadi kituoni. Aliliona vizuri gari lilivyokuwa limepaki na mtu yule walivyoshuka na kumfuata dada aliyekuwa na mtoto.

Hadi mtu yule alivyopanda kwenye gari alimuona vizuri zaidi. Na wala hakutetemeka sana na milio ya risasi kwa sababu eneo ambalo alikuwapo asingeweza kudhurika.

*************************

Anaitwa Jerry Mjanja. Ni kijana mwenye umri wa miaka 30 sasa. Alikuwa amepaki gari lake aina ya Toyota Probox jeupe. Alikuwa amepanda kwenye jengo moja la ghorofa nne. Alikuwa kwenye shughuli zake za kawaida.




**Wawili wale walivuka barabara na kwenda kituoni. Kiasi ilihisi wivu ukimshika. Alitamani yule mwanamume aliyekuwa ameongozana naye awe yeye. Dakika tatu baadaye alisikia milio mitatu ya bastola. Alishtuka, lakini ilionekana ni nje ya jengo alilokuwapo, hivyo alijiona yuko salama.**

Wakati akiwa ghorofa ya kwanza akielekea juu kwa ngazi, macho yake yalitua kwenye mwili wa mtu ambaye ni kama anamfahamu.

Ni kweli anamfahamu. Anaitwa Neema. Moyo wake ulishtuka. Miguu yake iligoma kuondoka alipokuwapo kumwangalia dada huyo.

Kichwa chake kilibeba nywele ndefu zilizosukwa kwa mtindo wa rasta zenye rangi za kahawia na nyeusi. Alivaa gauni la rangi ya bluu na kikoi chepesi cheusi kuanzia mabegani lakini kikiishia tumboni.

Kutokana na jua kuwa kali wakati huo aling'aa kama mbalamwezi kutokana na weupe wake. Alikuwa amebeba mtoto. Kingine kilichoonekana kama kumwumiza roho alikuwa ameongozana na mwanamume.

"Yaah! Aliniambia ameolewa." Alijisemea mwenyewe. Tayari alikuwa amesahau hata alikopaswa kwenda.

Alikuwa amesimama kwenye ngazi akizidi kuwakodolea macho, mwanamume na mwanamke aliyebeba mtoto.

"Kumbe ni kweli, hakunidanganya." Safari hii aliongea kwa sauti lakini kwa sababu hakukuwa mtu hapo hakuna aliyemsikia. Akili yake sasa ikamtuma asimame hapo hapo awaangalie hadi watakapoishia.

Wawili wale walivuka barabara na kwenda kituoni. Kiasi ilihisi wivu ukimshika. Alitamani yule mwanamume aliyekuwa ameongozana naye awe yeye.

Dakika tatu baadaye alisikia milio mitatu ya bastola. Alishtuka, lakini ilionekana ni nje ya jengo alilokuwapo, hivyo alijiona yuko salama. Mbele yake kulikuwa na vioo na ndivyo vilivyomfanya kuona yote hayo kwa usahihi.

Aliliona tukio lile la yule jamaa mrefu mweupe kumnyang'anya mtoto Neema vizuri sana. Alimwona yule jamaa akiondoka na kuingia kwenye gari. Kwa sababu alikuwa mbali kidogo na tukio na ndani ya jengo hakuwa na hofu sana. Na hiyo ndiyo iliyosababisha atoe simu yake ya kisasa na kuipiga picha za mnato na video gari ile haraka.

****************************************

Mawazo yalimrudisha nyuma Jerry. Akakumbuka kuwa miezi mitatu iliyopita alikutana na Neema maeneo ya Makumbusho. Alikuwa ameshuka kwenye gari lake kununua matunda. Hapo hapo macho yake yalikutana na mwanadada mrembo ambaye alipomwona tu, moyo wake ulilipuka. Hakujua ni kwa nini.

Jiji kubwa kama la Dar es Salaam lina wanawake wengi warembo. Wengine ni wazuri wa kuzaliwa, wengi wamejiongezea kwa vipodozi vinavyopatikana madukani.

Wote ukikutana nao huwezi kujua mrembo asili ni yupi na wa kutengeneza ni yupi.

Unayekutana naye hapa, ukigeuka unakutana na mwingine ambaye ni mzuri zaidi kuliko uliyekutana naya mwanzo.

Ukipiga hatua tano unawasahau wote wawili wa mwanzo, utakapokutana na mwingine ambaye anaonekana kuwazidi wote. Haya ni maisha ya kawaida na yamezoeleka.

Lakini kwa mrembo huyu Jerry alikuwa kama kuna nguvu fulani imemtoka mwilini. Ilikuwa ni kama amepigwa na shoti fulani. Haya mwenyewe hakujua sababu.

Baada ya kununua matunda alibaki amesimama. Aliganda kama vile amekunywa gundi.

Aliaga, lakini hakuondoka. Ni kama vile mtu aliyekuwa anasubiria mvua, wakati haikuwapo.

Jerry aliganda kwa sababu msichana huyo alionekana kuzungumza na muuza matunda, licha ya kwamba na yeye alikuwa tayari ameshanunua na kifuko chake amekishika mkononi.

Baada ya dakika kadhaa, msichana huyo alionekana kupiga hatua kadhaa akiondoka. Ndiyo fursa ambayo alikuwa anaitaka. Na yeye taratibu akaanza kuondoka. Ni kama walikuwa wanaogozana hivi, lakini kila mmoja alikuwa kwenye safari zake. Safari ya Jerry ikaishia kwenye mlango wa gari lake. Msichana alikuwa nyuma yake anataka kupita.

"Dada habari yako." Alimsalimia.

"Nzuri tu kaka." Msichana yule alijibu kwa haraka ambayo hakutegemea.

Mara nyingi wanawake warembo kama yule huwa wazito kujibu salamu hasa za mwanaume, kwa makusudi au kwa kuathirika na maneno wanayoambiwa kila wanapopita kuwa ni wazuri na warembo.

"Nimekuona pale nilipokuwa nanunua matunda."

"Eeeeh! Ni kweli na mimi nilikuwa nanunua matunda na nimekuona pale." Alijibu kama mtu ambaye wanafahamiana. Hili lilimshangaza mno Jerry. Lakini ni kama vile ilikuwa na faida kwake.

"Sasa dada, unaonaje nikikusogeza mbele unakokwenda."

"Mhh, mimi naenda mbali sana, nasubiri daladala hapa."

"Mbali wapite tena dada?"

"Keko." Jerry aliangua kicheko kifupi.

"Hapana wewe unapoishi si mbali. Ila mimi kwangu ndiyo mbali zaidi kuliko kwako."

INAENDELEA JUMAPILI

# DICKY FLAVOUR AOMBA MASHABIKI 'TUYAMALIZE'



MWANAMUZIKI chipukizi wa Bongo Fleva, Sadiki Piku, maarufu Dicky Flavour, ametambulisha video ya ngoma yake mpya inayoitwa 'Tuyamalize' ambayo imeanza kuwatikisa mashabiki wa muziki.

Akizungumza na Nipashe, Dicky amesema video ya wimbo huo imetayarishwa na Rifat na upande wa muziki umeandaliwa na prodyuza maarufu Zest ambaye ngoma zake zinaendelea kutesa ndani na nje ya Bongo.

"Wimbo wangu unazungumzia jinsi watu wanavyoweza kutatua matatizo yao na kwa amani na kurudi katika uhusiano wao, ni wimbo mzuri na wenye kufundisha zaidi," amesema Dicky.

Aidha, amesema baada ya kutambulisha wimbo wake huo na mashabiki kumuunga mkono, kuna mfululizo wa kazi zinafuata na kueleza zitakuwa bora zaidi na kuleta mapinduzi katika tasnia ya muziki nchini.

## Chin Bees alianzisha bifu kwa Country Boy

MSANIII wa muziki wa Hip hop, Chin Bees, amewaponda vikali Country Boy, Moni Centrozone na Young Lunya, kuwa hakuna anayeweza kujiita kuwa mwimbaji wa Trap.

Akizungumza hayo kupitia shoo ya Friday Night Live ya EATV, Chin Bees amesema mpaka sasa hajaona mtu anayefanya muziki wa Trap, labda watokee wasanii wapya.

"Mpaka sasa sijasikia mtu anafanya Trap ila naona watu wanarap, labda wakitokea wasanii wapya, lakini kwa sasa sioni mtu anayefanya muziki wa Trap."

Ameongeza "Kila kazi yangu ninayoitoa mimi inashika namba moja kuanzia kwenye Nesanesa, Nasebenza, Nyonga nyonga nimeanza zamani na sasahivi nina kampuni yangu ya BGE ndiyo maana kazi zangu za sasa ni tofauti na zamani".



## 'Don't Cry' ya Chidi Benz noma

MASHABIKI wa muziki nchini, wamepokea wimbo mpya wa rapa Chidi Benz, unaoitwa 'Dont Cry' kwa maoni tofauti.

Huko nyuma Chidi Benzi, alisema amefanya ngoma na mkali wa HipHop duniani, marehemu 2Pac Shakur ambaye amefariki dunia kwa kupigwa risasi 1996.

Watu wengi wamemsifu kwa ubunifu wake na kusema wimbo huo utampatia nafasi nyingine ya kutawala muziki wa kufokafoka kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.



HABARI MICHEZO

# Gallas ataka Arteta afukuzwe

**LONDON,** England

WILLIAM Gallas amesema Mikel Arteta "sio kocha sahihi" kwa Arsenal na ameiomba klabu hiyo imchukue kiungo wake wa zamani, Patrick Vieira.

Arteta anazidi kuiongezea presha Arsenal kufuatia matokeo mabaya, huku akipata ushindi mmoja tu katika mechi tisa za mwisho za Ligi Kuu England.

Kwa sasa Arsenal inashika nafasi ya 15 katika msimamo wa ligi hiyo wakiwa na pointi 15.

Gallas anasema Arsenal itakuwa inafanya makosa ikiwa wataendelea na Mhispania huyo.

Gallas amesema: "Ni nini kinachoendelea huko Arsenal? Ni swali ambalo nadhani kila mtu ameuliza msimu huu. Sijui jibu.

"Nadhani labda suala kwa sasa ni kwamba Mikel Arteta sio kocha sahihi. Kwangu yeye hana uzoefu huo wa kusimamia klabu kubwa.

"Pengine Vieira ana uzoefu mkubwa na hivyo nadhani yeye ndio anaweza kufiti pale, lakini sio Arteta."






# MBAPPE 'AOTA MBAWA' MADRID

**PARIS,** Ufaransa

USAJILI wa mshambuliaji, Kylian Mbappe kwenda Real Madrid kutoka Paris Saint-Germain upo shakani kwa mujibu wa gazeti la AS.

Mbappe mwenye umri wa miaka 22, amekuwa akihusishwa na uhamisho wa kwenda Madrid baada ya kung'ara akiwa na PSG, ambako mkataba wake unamalizika ifikapo mwaka 2022.

Lakini kufukuzwa kwa Thomas Tuchel kumeripotiwa kunaweza kuwa kizingiti cha Mbappe kutohamia kwa miamba hao wa mji mkuu wa Hispania.

Kwa mujibu wa ripoti, kuondoka kwa Tuchel kumekuwa ni pigo kubwa zaidi kwa Madrid kuipata saini ya mchezaji huyo.

Tuchel, alifukuzwa Alhamisi wiki hii na nafasi yake inatajwa kuchukuliwa na Mauricio Pochettino.

Mbappe amefunga mabao 14 katika mechi 18 alizoichezea PSG msimu huu.

# *Eriksen kubadilishwa kwa Van de Beek*

**MILAN,** Italia

KLABU ya Inter Milan imeripotiwa inafikiria uwezekano wa kufanya dili la mabadilishano kati ya nyota wa Manchester United, Donny van de Beek na Christian Eriksen.

Kwa mujibu wa ripoti kutoka Italia, nyota wa United, De Beek ameibuka kuwa windo la Milan.

Klabu hii kwa sasa inafanya tathmini ikiwa kuna uwezekano wa kufanya dili la mabadilishano.

De Beek ni zao la akademi ya vijana ya Ajax, alisajiliwa na United msimu wa joto uliopita, amekuwa sehemu muhimu sana ya kikosi cha Ole Gunnar Solskjaer.

Katika mechi zake 18 za United ilizocheza, ni mechi mbili tu za Ligi Kuu alizocheza.

Uamuzi wa nyota huyo kuhamia United ulikosolewa na baadhi ya wadau, akiwamo aliyewahi kuwa Kocha wa United, Louis van Gaal. Inter Milan wanataka kutumia mwanya huu kumchukua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23.

Hata hivyo, katika karata za uhamisho ambazo Inter Milan wanataka kuzicheza ni kuwapa ofa United ya dili la kubadilishana wachezaji, wakimtoa Ericksen ili wao wampate de Baek mapema Januari.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# KLOPP HANA HOFU HATIMA YA SALAH

Straika huyo ambaye yuko katika kiwango bora afunguka anataka kuendelea kuweka...

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp hajali wasiwasi juu ya mustakabali wa Mohamed Salah, akisisitiza mfungaji huyo anayeongoza katika Ligi Kuu England yuko "katika hali nzuri".

**Salah amekuwa katika kiwango bora kwa mabingwa watetezi wa ligi hiyo ambapo msimu huu, ameshafunga mabao 13.**

Ripoti ziliibuka wiki iliyopita kumhusisha Salah kutaka kuondoka Liverpool, ambaye alijiunga kutoka Roma mwaka 2017.

Mkataba wa sasa wa Salah - uliosainiwa mwaka 2018 - unaendelea hadi 2023, ingawa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 amedokeza anaona changamoto yake ijayo ni kuwa mbali na Merseyside, akimwambia Diario AS: "Nadhani Madrid na Barcelona ni klabu mbili kubwa.

"Nani anajua nini kitatokea siku za usoni, lakini hivi sasa nimezingatia kushinda Ligi Kuu tena na Ligi ya Mabingwa Ulaya nikiwa na Liverpool tena. "Kwa kweli nataka kuvunja rekodi hapa, narudia, rekodi zote za klabu, lakini kila kitu ni mikononi mwa klabu."

Raia mwenzake wa Misri, Mohamed Aboutrika amedai fowadi huyo, ambaye hivi karibuni alimzidi Steven Gerrard kama mfungaji bora wa muda wote wa Liverpool kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, hana furaha pale Anfield.

"Nilimpigia Salah simu kuhusu hali yake kule Liverpool na amesikitishwa, lakini hiyo haiwezi kuathiri utendaji wake uwanjani," alisema Aboutrika akinukuliwa na beIN SPORTS.

Lakini, alipobanwa juu ya hali ya Salah kabla ya mchezo wa nyumbani wa Liverpool dhidi ya West Brom, Jumapili, Klopp alisisitiza hakuna kitu cha kudokeza kwamba mchezaji huyo hafurahii kuwa Liverpool.

"Hatuzungumzii hadharani kuhusu mikataba, kwa nini tuanze sasa? Mo yuko katika hali nzuri, wakati mzuri, sura nzuri," Klopp alisema katika mkutano wa waandishi wa habari.

## ZISIKUPITE

### MESSI ATAJWA PSG

KOCHA wa zamani wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino, anataka kumsajili mshambuliaji wa Barcelona na Argentina, Lionel Messi (33), katika kikosi cha Paris St-Germain. Pochettino anatajwa kuwa kwenye nafasi ya kutua kwa mabingwa hao wa Ufaransa ambao hivi karibuni walimtimua Thomas Tuchel. ***(Le Parisien - in French)***

### CITY, STONES SAFI

MLINZI wa Manchester City na England, John Stones mwenye umri wa miaka 26, anatarajiwa kuongeza mkataba wa kuendelea kubaki pale Etihad baada ya kukubalika na kocha, Pep Guardiola msimu huu. ***(Telegraph)***

### ALABA NJIA MOJA

MLINZI wa Bayern Munich na Austria, David Alaba amekataa kusaini mkataba mpya na mabingwa hao wa Ulaya na anaweza kuzungumza na klabu mpya Januari. Chelsea, Real Madrid na Paris St-Germain zimeonyesha nia ya kuwania saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Mail)***

### ARSENAL YAMTAKA GOMEZ

ARSENAL ina nia ya kutaka kumsajili straika wa kimataifa wa Uruguay anayepiga pale Valencia, Maxi Gomez mwenye umri wa miaka 24. ***(Mirror)***

### DIGNE KIMEELEWEKA

EVERTON inaandaa mkataba mpya kwa mlinzi wake wa kushoto, Lucas Digne, 27, raia wa Ufaransa. Manchester City ni miongoni mwa klabu inayomwania. ***(Times)***

### ROJO AGOMBEWA

NEWCASTLE United na Sheffield United zinawania kumsajili kwa mkopo mlinzi wa Manchester United na Argentina, Marcos Rojo, 30. ***(The Athletic)***

### OBLAK ANUKIA PSG

KLABU ya Paris St-Germain inapanga kutoa ofa kwa Atletico Madrid kwa ajili ya golikipa wake, Jan Oblak, 27, huku raia huyo wa Slovenia akiwa anataka changamoto mpya. ***(Mail)***

### JONES AKARIBIA BROM

MLINZI wa Manchester United na England, Phil Jones, 28, anawaniwa kwa mkopo na West Bromwich Albion na Derby County. ***(Star)***

### UNITED YAMTAKA CAICEDO

MANCHESTER United inataka kumsajili kiungo wa Ecuador, Moises Caicedo mwenye umri wa miaka 19, kutoka Independiente del Valle wakati wa dirisha dogo la Januari. ***(Manchester Evening News)***

### GUARDIOLA: SISAJILI

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, hatarajii kusajili wachezaji wapya wakati wa dirisha dogo la Januari, licha ya Gabriel Jesus na Sergio Aguero wote waliukosa mchezo wa ushindi wa 1-0 dhidi ya Southampton, Jumamosi kuwa majeruhi. ***(Goal)***

HABARI MICHEZO

## Waziri Zanzibar awapongeza ZFF

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, amelipongeza Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), kwa uamuzi wake wa kuanzisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi kwa wanawake.

Waziri Tabia alitoa pongezi hizo juzi, wakati akifungua rasmi mashindano hayo katika Uwanja wa Mau B, ambapo Jumbi Queens na Womens Fighters zilitoka sare ya bao 1-1.

Alisema kuanzishwa kwa mashindano hayo kutaongeza hamasa kwa wasichana kuupenda mchezo huo, ikilinganishwa na hali ilivyo sasa.

Alisema pia yatachangia ongezeko la timu za wanawake na kuwaimarisha wachezaji kwa ajili ya kushiriki mashindano ya kimataifa pale Zanzibar itakapopata fursa ya kushiriki mashindano ya nje kama vile mashindano ya Kombe la Chalenji (CECAFA).

"Niipongeze (ZFF), kupitia kamati yake ya soka la Wanawake, wamewaza jambo zuri ambalo litasaidia hata kupata wachezaji wazuri watakaounda Timu ya Taifa ya Wanawake, mashindano haya pia yatasaidia kuwa na ligi nzuri ya wanawake," alisema Waziri huyo.

Kiongozi huyo alitoa mchango wa mipira 10 na kuahidi kusaidia katika bajeti ya Kamati ya Soka la Wanawake ili kuyafanya mashindano yafanyike katika mvuto na kiwango cha juu.

## Kiduchu aibuka kidedea Pangani

**Na Steven William,** PANGANI

BONDIA Dulla Kiduchu wa Muheza jijini Tanga, ameibuka mshindi dhidi ya Msingwa Daudi wa Pangani katika pambano lisilokuwa na ubingwa lililofanyika mjini hapa juzi usiku.

Kiduchu alitangazwa kuwa mshindi baada ya mpinzani wake Msingwa kuweka wazi hataweza kuendelea na pambano hilo lililofanyika pembeni mwa ufukwe wa bahari ya Hindi, ikiwa ni sehemu ya sherehe za sikukuu ya Krismasi.

Baada ya kumalizika kwa raundi ya kwanza, mabondia wote walikwenda mapumziko kwa ajili ya kupokea mbinu kutoka kwa makocha wao, lakini ilipogongwa kengele kuashiria kuanza kwa raundi nyingine, Msingwa aliwafuata majaji na kueleza hawezi kuendelea na pambano na kukubali Kiduchu atangazwe mshindi.

Awali kila bondia alionekana kujiandaa vyema na kupigana ngumi kwa kuviziana na kuwafanya mashabiki wa pande zote mbili kushangilia.

Hata hivyo, jambo la kushangaza, baada ya kengele kupigwa kwa ajili ya kuanza kwa raundi ya pili, Msingwa alinyoosha mikono mbele ya Kiduchu kuashiria amekubali kupoteza pambano hilo.

# IHEFU FC WAGENI BARA WANAOTAABIKA MKIANI

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MZUNGUKO wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara umemalizika na tayari idadi ya timu nyingi zimekamilisha michezo 17 ya awali, ukiachilia mbali zile zenye viporo vichache ambavyo vimesababishwa na wawakilishi wa nchi wanaoshiriki michuano ya kimataifa.

**Katika ligi hiyo, kwenye msimu huu wa 2020/21, Jiji la Mbeya linawakilishwa na timu tatu ambazo ni Mbeya City, Tanzania Prisons am bayo imeweka maskani yake ya muda mkoani Rukwa pamoja na wageni, Ihefu FC.**

Ihefu yenye maskani yake katika Mji wa Ubaruku wilayani Mbarali ni miongoni mwa timu zilizomaliza mzunguko wa kwanza zikiwa zinachechemea kwenye mstari mwekundu wa msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha klabu 18.

Nafasi ya timu hiyo kwenye msimamo wa ligi inatia wasiwasi endapo inaweza ikautumia vizuri mzunguko wa pili kujinasua mkiani na pengine kunusurika na janga la kushuka daraja.

Pamoja na timu hiyo kuwa katika nafasi mbaya kwenye msimamo, lakini ni miongoni mwa timu ambazo zimekuwa zikipata matokeo ya kusuasua ambapo mpaka sasa imekuwa zikipata matokeo kwa mbinde.

Mpaka sasa timu hiyo imeambulia vichapo kwenye michezo 10 kati ya 17 ambayo imecheza, sare nne na kupata ushindi kwenye michezo mitatu pekee, matokeo ambayo yanaifanya safari ya timu hiyo kuwa ya mashaka.

Hata hivyo Ihefu ni miongoni mwa timu zenye uwiano mbaya wa mabao ya kufungwa na kufunga, ambapo mpaka sasa imefungwa mabao 21 na kufunga saba pekee sawa na Mbeya City ambayo yenyewe imefungwa mabao 20.

Ushindi mkubwa ambao Ihefu iliupata kwenye Ligi Kuu tangu ilipopanda ni wa 2-1 dhidi ya Kagera Sugar, mchezo uliochezwa Desemba 14, mwaka huu, katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini hapa.

Ushindi mwingine ambao Mbogo Maji hao waliupata ni wa 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting ya mkoani Pwani maarufu kwa jina la 'Barcelona ya Bongo' ambao ndio ulikuwa ushindi wa kwanza pamoja na ushindi wa 1-0 dhidi ya Watoza Ushuru wa Kinondoni, KMC FC.

Lakini pamoja na timu hiyo kuambulia vichapo 10 na ushindi kiduchu imeonyesha kuwa safu yake ya ulinzi sio mbaya kwa sababu kichapo kikubwa ambacho timu hiyo imewahi kupokea ni cha mabao 3-0 ambacho ilipokea mara mbili.

Michezo ambayo timu hiyo ilipokea vichapo vya mabao 3-0 ni kutoka kwa Dodoma Jiji Fc Novemba 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Jamhuri ambao Ihefu ilikuwa mgeni pamoja na kichapo cha nyumbani kwenye mchezo wa mwisho wa mzunguko wa kwanza kutoka kwa vinara wa ligi hiyo, Yanga.

Vile vile timu hiyo imeonyesha kutumia vyema uwanja wa nyumbani ambapo michezo yote mitatu iliyoshinda, ilipata pointi tatu ndani ya Uwanja wa Sokoine (mechi mbili), na moja dhidi ya KMC ambao ulichezwa kwenye Uwanja wa Mbarali Estate.

Kati ya sare mbili ambazo Ihefu iliambulia kwenye mzunguko wa kwanza, mbili ilikuwa kwenye uwanja wake wa nyumbani wa Sokoine kati yake na Namungo ya mkoani Lindi pamoja na JKT ya mkoani Dodoma na sare zingine ambazo ni kati yake na Mbeya City pamoja na Polisi Tanzania ilikuwa ugenini.



Baadhi ya wachezaji na viongozi wa Yanga wakiwa na watoto yatima wanaolelewa katika kituo kilichoko chini ya Hospitali ya Mbozi Mission iliyoko mkoani Songwe walipowatembelea na kuwapa zawadi kwa ajili ya kusherehekea sikukuu ya Krismasi. **PICHA: MTANDAO**

## *Monzinzi azigonganisha Azam, Upopo*

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa Azam umesema umefanikiwa kumsajili mshambuliaji, Mpianza Monzinzi baada ya kuvunja mkataba wake miezi sita na klabu yake 'mama' ya Maniema na si FC Lupopo kama wanavyoyodai kuwa ni mchezaji wao halali.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zacharia, alisema taarifa zinazoenea kutoka kwa FC Lupopo kuwa mshambuliaji huyo bado ni mchezaji wao si sahihi na ni kauli za kuwatuliza mashabiki wao na si vinginevyo.

Zacharia alisema Monzinzi alikuwa akiichezea Lupopo kwa mkopo na Maniema ndiyo inayostahili kulipwa ada ya uhamisho na Azam wamefuata taratibu hizo.

"Huyu mchezaji amenunuliwa, na alikuwa amebakisha miezi sita. Kinachotokea sasa ni mkanganyiko wa upande wa FC Lupopo ambako alikuwa akicheza kwa mkopo. Huyu ni mchezaji wa Maniema FC ambako sisi ndiko tulikovunja mkataba," alisema Zacharia.

Aliongeza wachezaji wengi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), humilikiwa na watu binafsi, hivyo wao waliongea na mmiliki wa mchezaji huyo pamoja na klabu yake Maniema na baada ya kumalizana, walimpa mkataba wa mwaka mmoja.

"Hili jambo ni kama lile letu na Polisi Tanzania, tulipowapa Ditram Nchimbi, lakini baadaye tukamchukua na kumuuza Yanga, sisi ndiyo tulibaki kumalizana na Polisi Tanzania na wala si Yanga tena," alisema Zacharia.

Baada ya kuonekana kusuasua kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Azam FC imeamua kuimarisha kikosi chake katika kipindi cha dirisha dogo la usajili linaloendelea hapa nchini.

# Michezo

Jumapili Desemba 27, 2020

Nipashe




Klopp hana hofu hatima ya Salah UKURASA 22



Mshambuliaji wa kimataifa wa Simba, Meddie Kagere (kushoto), akiwa na Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Suleiman Matola, baada ya kuwasili nchini jana wakitokea jijini Harare, Zimbabwe katika mechi ya kimataifa ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya FC Platinum. Simba ilifungwa bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YASAKA HESHIMA FA

## ●●● Sven asisitiza ameandaa kikosi cha maangamizi dhidi ya Majimaji ili kutorudia...

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA watetezi wa mashindano ya Kombe la FA, Simba wanatarajia kuanza kutetea taji lao kwa kuwakaribisha Majimaji kutoka Songea katika mechi ya raundi ya tatu ya michuano hiyo itakayochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam.

**Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Mkuu wa Simba Mbelgiji, Sven Vandenbroeck, alisema mechi ya leo ni ngumu kwa sababu kila timu inahitaji ushindi na kusonga mbele katika mashindano hayo.**

Sven alisema wanatarajia kukutana na ushindani kwa sababu wapinzani wao wanawafahamu zaidi tofauti na yeye anavyokifahamu kikosi cha Majimaji inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza.

Kocha huyo alisema wamejipanga kuongeza umakini kila watakapokuwa na mpira, lakini pia wakiwaheshimu Majimaji kwa sababu ni timu yenye rekodi ya kuwasumbua vigogo wa soka nchini kila wanapokutana.

Alisema anatarajia kutumia wachezaji ambao hawakupata nafasi katika mchezo uliopita wa kimataifa dhidi ya FC Platinum, lakini kikubwa kuweka wachezaji watakaompatia matokeo chanya.

"Utakuwa mchezo mgumu, hakuna mechi nyepesi katika dunia ya sasa, timu zote zinaingia uwanjani kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri, sisi dhamira yetu ni kuendelea mbele na hatimaye kutetea ubingwa tulionao," alisema Sven.

Aliongeza matokeo mabaya ya mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika yatachangia kuufanya mchezo wa leo kuonekana wa 'kulipiza kisasi' ili kuwarejesha wachezaji kwenye nafasi yao ya mapambano.

Nahodha wa timu hiyo, John Bocco, aliliambia gazeti hili wamejipanga kuanza vyema michuano ya Kombe la FA kwa sababu wanajua inatoa tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa.

Bocco alisema kila mchezaji amejiandaa kucheza kwa kiwango cha juu kwa sababu hawataki kutolewa mapema katika michuano hiyo.

"Tuko tayari, tumejipanga kwa ajili ya kutafuta ushindi, tunajua haitakuwa kazi rahisi, lakini tunapenda kuwaambia mashabiki wetu wasiwe na wasiwasi, tutawapa furaha," Bocco alisema.

Ofisa Habari wa Majimaji, Godfrey Mvulla, alisema wachezaji wa timu hiyo hawana hofu yoyote kuelekea katika mchezo huo ingawa wanafahamu wanakutana na Simba yenye mashabiki wengi.

"Katika mpira lolote linaweza kutokea, tumejiandaa vizuri na tumewaambia wachezaji wetu kupata ushindi Jumapili (leo), ni jambo linalowezekana, kikubwa waongeze umakini," alisema Mvulla.

Mechi nyingine za mashindano hayo zitakazochezwa leo ni kati ya Mtibwa Sugar dhidi ya Geita Gold itayochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro, huku Namungo FC ikiwaalika Green Warriors Uwanja wa Azam Complex jijini.

Yanga tayari imetinga raundi ya nne ya michuano hiyo baada ya wapinzani wao, Singida United kushushwa madaraja mawili kutokana na kushindwa kutokea kwenye mechi yao ya Ligi Daraja la Kwanza dhidi ya Alliance FC ya jijini Mwanza.

## Yanga yabadili mipango Mbeya

**Na Saada Akida**

IKIWA ndio timu pekee iliyomaliza mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara bila ya kufungwa, Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze amesema amewaongezea dozi ya mazoezi wachezaji wake ili waanze mzunguko wa lala salama kwa kishindo.

Yanga itakuwa ugenini Alhamisi dhidi ya Tanzania Prisons katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa kwenye Uwanja wa Nelson Mandela Mjini Sumbawanga.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Yanga, Hafidh Salehe, alisema baada ya mapumziko ya siku tatu, kikosi chao kilianza tena mazoezi jana lakini sasa wakifanya kwa awamu mbili.

Saleh alisema lengo la Kaze kuongeza awamu nyingine ya mazoezi ni kuwajenga wachezaji na kuwaweka fiti na tayari na 'mbio' za lala salama.

"Tutakuwa na mechi ngumu na yenye ushindani mkubwa, kocha ameona mechi yetu ya kwanza ambayo tulitoka nao sare hivyo anafanyia kazi mapungufu yetu kuelekea mechi hiyo, wachezaji wanafanya mazoezi mara mbili kujiweka fiti zaidi," alisema Saleh.

Meneja huyo alisema wanahitaji kuanza duru la pili kwa kuondoka na pointi tatu, hivyo wanawaandaa wachezaji wao kukabiliana na ushindani dhidi ya 'Maafande' hao.

"Tunataka tuanze mzunguko wa pili kwa mwendo wao ni ule ule ambao tulimalizia katika mzunguko wa kwanza, ila safari hii tunataka kuongeza kasi.

"Prisons ni timu ya ushindani kwa sababu tulianza nao kufungua ligi msimu huu na kutoka nao sare uwanja wa nyumbani, sasa hivi tupo kwao, utakuwa mchezo mgumu kwa sababu kila mmoja wetu anahitaji kupata matokeo chanya," aliongeza.

Alisema wachezaji wote walioko jijini, Mbeya wako vizuri, hakuna majeruhi na kila mmoja yuko tayari kwa ajili ya mchezo huo.

Yanga ndio vinara wa Ligi Kuu Bara wakiwa na pointi 43 wakifuatiwa na watani zao na mabingwa watetezi, Simba wenye pointi 32 lakini wakicheza mechi tatu pungufu.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 3 9

9 770856 541002 >